Jumamosi Machi 12, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580882

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

SportPesa
TZS. 1,013,643,920
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#



**PM** azionya NGO uchochezi migogoro Hifadhi Ngorongoro UKURASA 3




**POGBA, MAN UNITED MAMBO MAGUMU** UKURASA 21

BAJETI 2022/23

# Watumishi kuongezwa mishahara

• **Makandarasi** nao wakumbukwa, serikali yapanga kukusanya, kutumia tril. 41.06/-... *Endelea ukurasa 2*




## Kitendawili ujenzi stendi ya Mwenge chateguliwa

UKURASA 3



## Shoo ashauri serikali kusaidia chakula kaya 3,700 wafugaji

UKURASA 2

**MICHEZO** PABLO AFUNGUKA SIMBA IMETIMIA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza Kikao Maalum cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Watumishi kuongezwa mishahara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI katika bajeti ya 2022/23, inatarajiwa kukusanya na kutumia Sh. trilioni 41.06 zikiwamo Sh. trilioni 9.74 kwa ajili ya nyongeza za mshahara na upandishaji madaraja watumishi wa umma.

Bajeti hiyo ambayo ni ongezeko la asilimia 8.1 ikilinganishwa na ya 2021/22 ya Sh. trilioni 37.98, imezingatia mahitaji ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ikijumuisha ulipaji wa deni la serikali, ajira mpya, sensa ya watu na makazi pamoja na kugharamia miradi mikubwa ya maendeleo.

Aidha, bajeti hiyo inatarajiwa kuwa ya kihistoria katika kilimo kutokana na mipango mikubwa kuelekezwa katika kilimo cha umwagiliaji.

Akiwasilisha mapendekezo ya serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 na mfumo wa ukomo wa bajeti kwa wabunge jana, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 28.69 sawa na asilimia 69.9. Kati ya hayo, mapato yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 11.1 hadi Sh. trilioni 24.19 kutoka Sh. trilioni 21.77 mwaka 2021/22.

"Mapato yasiyo ya kodi (wizara, idara, taasisi na mamlaka za serikali za mitaa) yanakadiriwa kuongezeka hadi Sh. trilioni 4.50 mwaka 2022/23 kutoka Sh. trilioni 3.91 mwaka 2021/22," alisema.

Waziri pia alisema misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo inatarajiwa kufikia Sh. trilioni 4.15, sawa na asilimia 10.1 ya bajeti yote.

Pia alisema serikali inatarajia kukopa Sh. trilioni 5.35 kutoka soko la ndani zikiwamo Sh. trilioni 3.3 kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za serikali zinazoiva na Sh. trilioni 2.054 kugharamia miradi ya maendeleo.

Kwa mujibu wa Waziri, serikali inatarajia kukopa Sh. trilioni 2.85 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu.

**DENI LA SERIKALI**

Dk. Mwigulu alisema kwa mwaka 2022/23, serikali inapanga kutumia Sh. trilioni 25.54 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni asilimia 62.2 ya bajeti yote, ikijumuisha Sh. trilioni 11.30 kwa ajili ya ulipaji wa deni la serikali na gharama zingine za mfuko mkuu.

"Pia Sh. trilioni 9.74 kwa ajili ya mishahara ikiwamo nyongeza za mshahara, upandishaji wa madaraja kwa watumishi na ajira mpya. Aidha, Sh. trilioni 4.49 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ikijumuisha Sh. bilioni 200 kulipa madeni yaliyohakikiwa ya watumishi na wazabuni,"alisema.

**MIRADI YA MAENDELEO**

Waziri alisema serikali imepanga kutumia Sh. trilioni 15.52 sawa na asilimia 37.8 ya bajeti yote kwenye miradi ya maendeleo. Sh. trilioni 12.12 ni fedha za ndani, sawa na asilimia 78.1 ya bajeti ya maendeleo na Sh. trilioni 3.39 ni fedha za nje.

"Fedha za maendeleo za ndani zinajumuisha kugharamia mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha 'standard gauge, mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere, Mfuko wa Barabara, mifuko ya reli, maji na REA," alisema.

Pia alisema Sh. bilioni 558 zitatumika kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, Sh. bilioni 400 kulipa malimbikizo ya madeni yaliyohakikiwa ya makandarasi na Sh. bilioni 393.3 kwa ajili ya kugharamia elimu msingi bila ada.

**MIRADI KIELELEZO**

Alisema Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 utajumuisha uendelezaji wa miradi ya kielelezo ambayo inatarajiwa kuwa na matokeo mapana na ya haraka katika uchumi.

Miradi hiyo ni ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR), Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115, Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania), Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) - Lindi na kuendeleza Kanda Maalumu za Kiuchumi ikiwemo Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo.

**MAENEO YA KIPAUMBELE**

Alisema Miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2022/23 itazingatia maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 ambapo miradi itakayotekelezwa itajikita katika kuchochea uchumi shindani na shirikishi.

"Miradi ya kipaumbele 2022/23 kwenye uendelezaji wa bandari italenga uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwa kuendelea kuongeza kina na kupanua lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli, kufunga na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na mifumo ya TEHAMA na kuimarisha miundombinu ya reli kwa ajili ya kusafirisha mizigo kwa njia ya reli Sh. bilioni 175.6 ya fedha za nje na Sh. bilioni 243.1 fedha za ndani zimetengwa,"alisema.

Alitaja eneo lingine ni kuimarisha uwezo wa uzalishaji kwenye Sekta zinazotoa malighafi Viwandani ili kukabiliana na viashiria hasi vya Deni la Taifa, ili kuendelea kuongeza pato la mtu mmoja na kupandisha nafasi ya Tanzania kwenda uchumi wa kati wa juu na kuongeza ajira.

Dk. Mwigulu alitaja eneo la tatu ni Kukuza Biashara na Uwekezaji kwa kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara ikiwemo kuimarisha mazingira ya kisera na sheria kuhusu uwekezaji pamoja na mifumo ya uratibu na usimamizi wa masuala ya uwekezaji kitaifa.

# Shoo ashauri serikali kusaidia chakula kaya 3,700 wafugaji

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, ameishauri serikali kuchukua hatua za haraka, kunusuru maisha ya kaya 3,738 za jamii za kifugaji zinazotishiwa na njaa.

Aidha, amemsihi Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kuielekeza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), kupeleka chakula cha msaada kwa wananchi hao walioathiriwa na ukame katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro.

Idara ya Diakonia ya Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT inayosimamia Huduma ya Yatima (HUYAMWI) na Kanisa la Kilutheri la Bavaria la Ujerumani, zimetafuta fedha Euro 4,000 zilizowezesha kupata chakula magunia 108 ya mahindi na 23 ya maharagwe.

Akizungumza jana katika Kijiji cha Tindigani, katika Kata ya KIA, Wilaya ya Hai, alipokwenda kuzindua mgawo wa chakula na miradi midogo ya mifugo, Askofu Dk. Shoo alisema:

"Kwa vyovyote vile ni muhimu chakula kutoka maghala ya taifa au hifadhi ya taifa ya chakula, kufikiria kupeleka chakula katika maeneo yote yaliyoathirwa na ukame (Wilaya za Simanjiro, Kiteto, Longido na Hai), na watu wauziwe chakula kwa bei ambayo wanaweza wakamudu.

"Na sisi kanisa kama sehemu ya utume wetu, tumeona umuhimu wa kuwasaidia hawa wenzetu walioathirika kutokana na upungufu wa chakula. Tumegawa chakula hiki ambacho kimechangwa kutoka Sharika za Milimani ambako wana nafuu kidogo, lakini pia tumepata msaada kutoka kwa rafiki zetu wa Ujerumani.

Kuhusu mabadiliko ya tabianchi kuitesa mikoa mbalimbali nchini, Askofu Dk. Shoo alisisitiza, "Ukame huu tunaoushuhudia, tunasema extreme drought ni sehemu ya matokeo au madhara ya kile tunachokiita mabadiliko ya tabianchi. Tutaendelea kushuhudia haya au hali kama hii kwa kipindi kirefu kama hatutajali jambo la utunzaji wa mazingira. Mabadiliko ya tabianchi yataendelea kuwa na athari kubwa sana hasa katika maeneo kama haya ya kwetu na ukanda wa bahari."

Awali, Mkurugenzi wa Huduma ya Yatima (HUYAMWI) ya Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT, Mdiakonia Samwel Mori, alisema awamu ya kwanza ya msaada huo ilikuwa magunia 64 za mahindi na 17 za maharagwe ambayo yaligawanywa katika Sharika za Nomeuti, Rundugai na Kawaya.

"Sharika hizi zilipatwa na njaa na uhaba mkubwa wa chakula uliosababishwa na ukame uliotokana na kukosekana mvua mwaka 2021, ukame uliendelea hadi Januari mwaka huu. Hali hii ilisababisha jamii nyingi kuishi maisha ya shida na njaa," alisema Mori.

Claus Heim ambaye ni Katibu Kanisa la Evangelical Lutheran Bavaria la nchini Ujerumani, baada ya kufikisha msaada huo katika vijiji vitatu vya Tindigani, Sanya Station na Mtakuja alisema;

"Sisi Kanisa la Kiinjili la Kilutheria Bavaria, tuna uhusiano na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, hasa Dayosisi ya Kaskazini. Hiki sio chakula tu, mahindi au maharagwe ila ni alama ya upendo na uhusiano. Kwa sababu Biblia imetufundisha kama upande mmoja ndani ya familia wanapata shida, hata upande mwingine wanapata shida," alisisitiza Heim.

Akishukuru kwa niaba ya wananchi hao, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Tindigani, Richard Moringe, alisema amefarijika wananchi wake kupata msaada wa chakula.

"Nimeona mkono wa kanisa katika chakula, kutuchimbia kisima kirefu cha maji na kutujengea kanisa. Nimefarijika sana kusikia chakula kimetolewa na Wajerumani. Nimefurahi Baba Askofu amewasiliana na uongozi wa Wilaya na wamenipigia wakaniambia kuna watu wanakuja wa kanisa wanaoshirikiana nao," alisema Moringe.

## Ugonjwa wa figo bado tishio kwa Watanzania

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

UGONJWA wa figo umeelezwa kuwa bado ni tishio kwa Watanzania wengi kutokana na kuambatana na maradhi mbalimbali.

Takwimu mpya zinaeleza kuwa asilimia saba ya Watanzania wana ugonjwa huo huku wengi wao wakiwa na shinikizo la juu la damu, kisukari na maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU).

Hayo yamebainishwa jana mjini hapa na Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Alfelo Sichwale, huku akisema takwimu hizo ni kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2013 kwa Tanzania.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Figo Duniani yaliyofanyika kitaifa Kibaha, mkoani Pwani, Dk. Sichalwe alisema takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kuwa asilimia 10 ya watu wote duniani wanaishi na ugonjwa sugu wa figo.

Alisema tatizo ni kubwa zaidi kwa watu wenye umri wa zaidi ya miaka 75 na asilimia 50 ya watu hao wana ugonjwa wa figo.

Aidha, alisema utafiti unaonyesha kati ya asilimia 11 hadi 17 ya watu wote wanaoishi Afrika hususani Kusini mwa Jangwa la Sahara wana ugonjwa wa figo.

"Tafiti (utafiti) zimebaini (umebaini) kuwa takribani Watanzania 5,800 mpaka 8,500 wanahitaji huduma ya kusafisha damu au kupandikiza figo na hadi kufikia Januari 31, mwaka huu, wagonjwa 2,750 sawa na asilimia 32 wanapata huduma ya kusafishwa damu huku wengine 325 wakipandikizwa figo," alisema.

Alisema kati ya waliopandikizwa figo, 93 wamepandikiziwa hapa nchini na Hospitali ya Taifa Muhimbili imepandikiza wagonjwa 67 na Benjamin Mkapa ya Dodoma wagonjwa 26.

Dk. Sichalwe alisema huduma za figo hususan za usafishaji wa damu (dialysis) zimekuwa zikitolewa na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, pamoja na hospitali za kanda na hospitali maalum, mkakati wa kupanua huduma hizo serikali imeendelea kuzijengea uwezo hospitali za rufani za mikoa kutoa huduma za usafishaji figo.

Kwa mujibu wa Mganga Mkuu wa Serikali, awamu ya kwanza ya utekelezaji imekamilika na serikali imeanzisha huduma za uchujaji damu (dialysis) kwenye hospitali za mikoa saba kwa kuzipatia mashine 49 na kukarabati majengo kwa gharama ya Sh. bilioni 2.8.

Hospitali za rufani za mikoa zilizoanzisha huduma hizo zimetajwa kuwa ni Mtwara, Arusha, Tanga, Kigoma, Kagera, Mara na Mwanza na mpaka sasa wagonjwa zaidi ya 150 wamefaidika na huduma hizo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Tumbi, Aman Malima, alisema Pwani ni mkoa unaotajwa kuongoza kwa kuwa na wagonjwa wa figo.

Alisema katika maadhimisho hayo ambayo yaliambatana na utoaji wa huduma za kupima afya bure kwa wananchi, 100 waliopima wamegundulika kuwa na dalili za ugonjwa wa figo.

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, alishukuru maadhimisho hayo kufanyika katika wilaya yake na kutoa fursa kwa wananchi kupima afya bure.

Baadhi ya wananchi waliopima wameishukuru serikali kwa utaratibu huo huku wakiomba iwe inafanyika mara kwa mara ili wananchi wengi wapate fursa hiyo na kujua maradhi yanayowasumbua na yatibiwe kwa wakati.

# Kitendawili ujenzi stendi Mwenge chateguliwa

**Na Romana Mallya**

MIRADI mitatu ya Manispaa ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam iliyosimama takribani miezi tisa ukiwamo wa ujenzi wa kituo cha daladala na uwanja wa michezo Mwenge, inatarajiwa kuanza tena wiki mbili zijazo.

Mbali na miradi hiyo, mradi mwingine unaotarajiwa kuanza tena ujenzi ni wa jengo la utawala la manispaa hiyo.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Hanifa Suleiman, alisema kwa sasa wako katika hatua za mwisho za kukamilisha ili kuendelea na ujenzi baada ya kusimamishwa Juni 20, mwaka jana, kwa agizo kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wakati huo, Ummy Mwalimu, ili kupisha uchunguzi.

"Waziri Ummy aliisimamisha na baadaye tume ya uchunguzi ilifanya kazi yake na yako maelekezo yamekuja kama Manispaa tunayatekeleza. Kwa sasa tuko katika mchakato wa kumpata mkandarasi ambaye atakamilisha miradi hii," alisema.

Kuhusu mkandarasi ambaye alikuwa akijenga majengo hayo hadi kusimamishwa, alisema wataendelea naye huku wakiwa na mtaalam ambaye atahusika kwenye maeneo yanayohitaji utaalamu zaidi.

"Mradi wa Mwenge utaanza hivi karibuni tulikamilisha utaratibu wake wiki iliyopita. Wiki mbili kuanzia sasa mradi utaendelea na ujenzi," alisema.

Alisema jana kamati ya zabuni ilikaa kupitia wazabuni ambao walichujwa na utaratibu utakaofuata ni wa bodi ya zabuni kukaa kwa hatua za mwisho.

Alisema mradi huo ambao unatakiwa kukamilika Juni, mwakani, watahakikisha unakuwa tayari kabla ya muda huo.

"Kutokana na kasi tunayokwenda nayo ndiyo maana tunataka mkandarasi mwenye uwezo kwa sababu tunajenga miradi hii kwa mapato yetu ya ndani ukikusanya unatenga ndipo unatekeleza, hivyo tunamtaka mkandarasi mwenye uwezo ambaye atakamilisha ndani ya muda mfupi huku ukusanyaji wa mapato ukiendelea," alisema.

Kiongozi huyo alisema mradi wa kituo cha daladala Mwenge utakapokamilika utakuwa na uwezo wa kuchukua zaidi ya wafanyabiashara 200 huku uwanja wa mpira ukichukua karibu watu 5,000 na pia utakuwa na maduka kuzunguka eneo hilo.

"Namna watu watakavyoingia, kuna utaratibu uliokuwapo ambapo wale wafanyabiashara ambao awali walikuwapo pale kabla, watapewa na wengine watapata yale yatakayobaki kwa utaratibu utakaowekwa kwa kuomba," alisema.

Juni, mwaka jana, Waziri Ummy alimsimamisha kazi Mhandisi Isack Mpaki anayesimamia miradi hiyo mitatu kwa kile alichodai kutoridhishwa na mwenendo wa ujenzi wake.

Ummy alichukua hatua hiyo baada ya kutembelea ujenzi wa mradi wa kituo cha mabasi Mwenge unaojengwa na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) kwa mfumo wa 'Local Fund' (Force Account) ambao ulianza Aprili, mwaka juzi.



Ofisa Msimamizi wa Kodi Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Julieth Shehiza (kulia),akitoa elimu ya kodi kuhusu umuhimu wa kutunza kumbukumbu za biashara kwa mfanyabiashara wa duka la nguo, wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi ya mlango kwa mlango, mkoani Dodoma mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PM azionya NGO uchochezi mgogoro Ngorongoro

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema vikao viwili vinatarajiwa kufanyika kwa ajili ya kutatua mgogoro ulioko kwenye Hifadhi ya Ngorongoro huku akitoa onyo kwa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO's) yanayochochea hali hiyo.

Akitoa maelezo ya serikali kwa wabunge jijini hapa jana, Waziri Mkuu alisema katika eneo la Tarafa ya Loliondo ambalo lina mazingira tofauti na liko kwenye mazalia ya chanzo cha maji amekamilisha mazungumzo kupitia vikao vitatu vilivyofanyika.

Hata hivyo, aliwataka wanasiasa walioko nje ya eneo la Ngorongoro waiache serikali izungumze na wananchi walioko katika maeneo hayo ili elimu na uhamasishaji wa wanaotaka kuhama kwa hiari wafanye wenyewe bila kushinikizwa na mtu yeyote na ambao wako tayari kuhama wasizuiwe. "Tunazo pia NGO's ambazo zenyewe zimejikita kutetea hifadhi ile iharibike, nakusudia kukutana nao tuwaelimishe na wao, tusikie wao wanasema nini, wanapotetea kuwa na idadi kubwa ya watu, wanataka nini, wanapenda uhifadhi au hawapendi uhifadhi, lakini pia tutazichuja maana nyingine sio za hapa nchini." "Nyingine zimekuja nchini kwanza kwa njia za kinyemela na hawa tukiwagundua tutahangaika nao, lakini wale waliopo nchini tutaangalia nani amesajiliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani, hawa tutakaa nao kama serikali kwa kuwa tuliwasajili wafanye shughuli zao," alisema.

Majaliwa alisema kwenye Tarafa ya Ngorongoro kama hali itaendelea kubaki ilivyo iko hatari kubwa ya hifadhi kuporomoka.

Alitaja sababu hifadhi hiyo kuporomoka kuwa ni idadi ya watu kuongezeka ambayo inakadiriwa kuwa 110,000.

"Idadi ya mifugo ni mingi mno sasa hivi inakadiriwa kuwa na mifugo 813,000, lakini pia ujenzi wa nyumba umeongezeka tena holela na uwepo wa nyumba za kudumu, haya yanapelekea uwepo wa hali ya hatari ya kutoweka ukiangalia ni maeneo ambayo taifa limepata heshima na dunia inaitambua," alisema. Kuhusu majina, alisema serikali imepokea orodha ya majina ya awali ya kaya 86 zenye watu 453 ambao wamekubali kuondoka kwenye Hifadhi ya Ngorongoro kwa hiari yao huku wengine wakiendelea kujiandikisha.

"Serikali imetenga eneo la hekari 400,000 lililoko katikati ya maeneo ya wilaya za Handeni, Kilindi, Kiteto na Simanjiro na hekari 220,000 tayari zimepimwa viwanja 2,406 kati ya hivyo, viwanja 2,070 tumeandaa kwa ajili ya makazi na kila kimoja kina ukubwa wa ekari tatu. Tumeanza na nyumba 101 zenye vyumba vitatu vya kulala kwa wale wanaotaka. Tuna viwanja 336 kwa ajili ya huduma kama shule za msingi na sekondari, zahanati na vituo vya afya, ujenzi wa mifumo ya maji kazi inaendelea."

"Kila mwananchi atapewa eneo la heka tatu ili aweze kujenga boma na kuwa na eneo la ufugaji, eneo hili lina hali ya hewa nzuri na linaweza kulisha mifugo msimu wote wa masika na kiangazi," alisema.


J & J RECOVERIES

P. O. Box 25637, Dar es Salaam, GOBA njia nne, Matosa road, Tanzania.

Date: 08/03/2022

NOTISI/TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **KITAMBAA CHEUPE MICROFINANCE LTD** iliyoko Goba senta,Dar es salaam, **J & J RECOVERIES** tunatangaza Mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa madeni yao Kuanzia tarehe 20/03/2022 na kuendelea kama ifuatavyo;

| SN | DHAMANA | MKOPAJI/MDAIWA | MMILIKI WA DHAMANA | ENEO HUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA | FRANCISCA FRANCE LEMINGE | MILLARD MSAMO MUSHI | MSIGANI, UBUNGO |
| 2 | KIWANJA | WILLIAM JEREMIAH NGUJI | WILLIAM JEREMIAH NGUJI | MSAKUZI,UBUNGO |
| 3 | NYUMBA | PAULINE JUSTINE SAMBA | PAULINE JUSTINE SAMBA | MAKABE,UBUNGO |
| 4 | NYUMBA | SALMA ALLY HAJI | SAID MNJINJO | VIJIBWENI,KIGAMBONI |
| 5 | NYUMBA | CLARA JOSEPH MAGESA | CLARA JOSEPH MAGESA | VIJIBWENI,KIGAMBONI |
| 6 | KIWANJA | HAPPY MBOGELA EKSON | HAPPY MBOGELA EKSON | MSANGANI,PWANI, KIBAHA |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% tarehe hiyo hiyo baada ya mnada kuisha na 75% italipwa ndani ya siku 14.
2. Gharama za kubadili umiliki wa dhamana ni za mnunuzi na dhamana zitauzwa Kama zilivyo.
3. Hati ya manunuzi(Certificate of sale) itatolewa kwa mnunuzi (highest bidder) baada ya kumaliza 75%

**Kwa mawasiliano zaidi piga; Piga simu: +255 714292260 / 0767148298 / 0718802350 / 0784076588**

116746502

HABARI KITAIFA

# TRA yawabana wafanyabiashara wasio na mashine za EFD

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imebaini uwapo wa baadhi ya wafanyabiashara ambao hawatumii Mashine za Risiti za Kielektroniki (EFD) na kuwataka wazinunue ili watoe kwa wateja wao na serikali ipate mapato yake.

Ofisa Mkuu Msimamizi wa Kodi wa TRA, James Ntalika, alielekeza hilo juzi mjini Dodoma wakati wa mwendelezo wa kampeni ya utoaji elimu kwa mlipakodi ya kuwatembelea wafanyabiashara katika maeneo yao ya biashara maarufu 'Mlango Kwa Mlango' ili kuwasikiliza na kutatua kero walizonazo.

Ntalika alisema katika kampeni hiyo wamebaini baadhi ya wafanyabiashara hawana EFD kitendo kinachokwamisha mamlaka kukosa mapato yatokanayo na biashara.

"Kuna baadhi yao hawana Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) tunawataka mfike Ofisi ya TRA mkoani hapa ili mkasajiliwe na kupatiwa TIN. Wapo wafanyabiashara hapa Dodoma ambao wanastahili kuwa na mashine za EFD, lakini mpaka sasa hawana," alisema.

Katika mkutano huo, wafanyabiashara wameiomba serikali ipunguze baadhi ya kodi kutokana na biashara zao kuwa ngumu na wengine walipongeza TRA kwa kuhimiza wananchi matumizi ya programu ya 'Hakiki Stempu'.



Mwanasiasa na mbobezi wa masuala ya maendeleo ya watu, Dk. Mayrose Majinge, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, wakati akimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa mafanikio makubwa ndani ya mwaka mmoja wa uongozi wake. **PICHA: ROMANA MALLYA.**

# Aomba Watanzania kumtia moyo Rais Samia

Na Romana Mallya

ALIYESHIKA nafasi ya tatu katika mchujo wa kumpata mgombea wa Urais wa Tanzania mwaka 2020 kupitia CHADEMA, Dk. Mayrose Majinge, amewataka Watanzania kumtia moyo Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya.

Dk. Majinge aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani na sheria ya mvuto ambayo falsafa yake huleta matokeo mazuri katika maisha.

Alisema katika mwaka mmoja wa Rais Samia aliokaa madarakani, amefanya makubwa ambayo yanastahili pongezi.

"Tunapotafakari mwaka mmoja wa Rais Samia, tupate muda wa kujitafakari kila mmoja, Je, tumekuwa wenye matumaini au waliokata tamaa, tumuangalie Rais kwa matumaini ili tuweze kunufaika na mazuri yake ambayo ni mengi. Kanuni ya dhahabu ituongoze," alisema.

Dk. Majinge ambaye pia amebobea katika masuala ya maendeleo ya watu alisema kwa muda mrefu imekuwa ni hulka ya jamii kuwa na tabia ya kubeza na kuwa na ari ya kusubiria mambo mabaya yatokee kwa wengine hasa kwa mtu anayefanya jambo jipya au aliyepata nafasi.

Alisema kuwa Watanzania hawawezi kujenga jamii bora kwa kushushana, kubezana, kudharauliana na kudhalilishana.

"Rais Samia wakati anaingia madarakani tulishuhudia baadhi walidhania hataweza sababu ni mwanamke, tabia ya kudhania mabaya imekuwapo katika jamii kwa muda mrefu na hufifisha umoja na kudumisha unafiki, ni tabia inayochangia kurudisha nyuma maendeleo," alisema.

Dk. Majinge aliwakumbusha watanzania kuwa ili kuwa na maisha bora, wanapaswa kuwa makini na wanavyofikiri na kauli wanazotoa.

"Maisha mazuri hutokana na jamii bora, hatuwezi kujenga jamii bora kama tunatabia ya kushushana na kubezana, kwa mujibu wa sheria ya mvuto siyo sahihi kuchukua au kuishi na fikra potofu," alibainisha.

Pia, alisema ipo kanuni ya dhahabu ambayo inataka mtu amtendee mwenzake vile anavyopenda kutendewa.

"Ninaomba tutumie ukurasa huu mpya ambao Mungu ameutoa kwetu Watanzania kwa kutupa kiongozi mwanamke, tujipange upya kifikra ili tufurahie maisha kwa kufanya taifa kuwa mahali pazuri pa kuishi na kufurahi," alisema.

Alisisitiza kuwa ikiwa matumizi bora ya sheria ya mvuto na kanuni ya dhahabu Watanzania wataondokana na fikra hasi, kutiliana mashaka, kuogopana, kunyoosheana vidole, kulaumiana na kuchukiana.

Dk. Majinge alisema lazima jamii ijiondoe kwenye tabia ya kuona mambo mabaya zaidi kuliko mazuri.

"Tusipende kuzungumzia mambo mabaya ya watu ama kuwadhania vibaya kufanya hivyo inajitupunguzia wenyewe ukaribu nao, mti unaouchukia huwezi kula matunda yake maana hautautunza ili ule matunda yake.

# Waziri atoa tamko stendi mpya Ilemela

Na Munir Shemweta

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka wananchi wa Ilemela kutunza miundombinu ya stendi mpya ya mabasi na maegesho ya malori Nyamhongolo iliyoko Manispaa ya Ilemela iliyokabidhiwa hivi karibuni kwa halmashauri hiyo.

Amesema utunzaji miundombinu hiyo utaiwezesha stendi hiyo kudumu kwa muda mrefu na kubainisha kuwa uharibifu wowote utakaofanyika utakifanya kizazi kijacho kutokuwa na manufaa nayo.

"Ukisikia historia ya mradi huu, serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imewatendea haki wana Ilemela. Tunamshukuru sana yeye pamoja na Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela aliyepita, John Wanga na timu yake, sambamba na Mstahiki Meya Renatus Mulunga na madiwani kwa kuhakikisha mradi umekamilika na kuanza kufanya kazi," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri Mabula, mradi huo wa stendi na maegesho ya malori una fursa mbalimbali zitakazowawezesha wananchi wa Ilemela na jamii nzima kufanya shughuli za kiuchumi kwa maendeleo yao, mkoa na taifa kwa ujumla.

Akizungumza katika mahojiano maalum na mwandishi wa habari hii jana, jijini Dodoma, Dk. Mabula alisema kipindi ambacho Rais Samia ameingia madarakani, ameendelea kufadhili mradi huo uliogharimu takriban Sh. bilioni 26.3.

"Ninachoweza kuwaeleza wananchi wa Ilemela, mradi ule ni wa kimkakati na utanufaisha wana Ilemela, watu wa Mwanza lakini pia na jamii kwa ujumla kwa sababu mabasi yatakayokuwa yakiingia na kutoka ndani ya stendi yatakuwa yakitoka mikoa mbalimbali," alisema.

Alisema stendi hiyo na maegesho ya malori ni ya aina yake na imesheheni huduma mbalimbali kama vile huduma za benki, maduka madogo ya bidhaa (mini supermarket) na migahawa itakayowawezesha wananchi kupata huduma pale wanapozihitaji.

"Stendi imewekwa maduka takriban 74 ili kuwawezesha abiria wanaoshuka kununua vitu huku wenye mabasi wakitengewa ofisi kwa ajili ya kutoa huduma," alisema.

Akizungumzia fursa za wafanyabiashara wadogo, maarufu kama wamachinga katika stendi hiyo, Waziri huyo ambaye ni Mbunge wa Ilemela, alisema Manispaa ya Ilemela ina mpango wa kujenga jengo kwa ajili ya machinga kufanya shughuli zao.

"Wamachinga nao watakuwa na jengo lao pembeni ya stendi maana mradi huu umekwisha na sasa tunategemea kuanza mradi mwingine wa machinga jirani na stendi," alisema.

"Tunajua eneo kama hili wamachinga wanahitaji kufanya biashara kwa kuwa ni stendi ya kisasa na mpango tulio nao kama wana Ilemela, tuna kiwanja kitakachojengwa 'machinga complex'," alisisitiza.

# Samia apongezwa kuinua sekta usafirishaji

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amepongezwa kwa kuimarisha uhusiano mzuri wa kidiplomasia na nchi jirani hali ambayo imesababisha kukuza biashara hasusani kwenye sekta ya usafirishaji.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Mwenyekiti wa Kundi la Kampuni za Simba Bingwa, Azim Dewji, akitoa tathmini ya kuelekea mwaka mmoja wa Rais Samia tangu alipoingia madarakani.

"Katika kipindi cha mwaka mmoja madarakani, Rais Samia amekuwa na mchango mzuri katika kuimarisha uhusiano mwema na nchi majirani, hivyo kusababisha biashara kuimarika," alisema Dewji wakati wa tathmini hiyo iliyoambatana na hafla ya kukabidhi tuzo kwa madereva bora wa kampuni hiyo kwa mwaka 2021.

"Mara nyingi ndugu yako wa damu ni jirani yako, kwa hili la Rais kuimarisha uhusiano mzuri na majirani zetu ni jambo jema sana ambalo limewezesha kuimarisha biashara hasa katika sekta ya usafirishaji," aliongeza.

Alisema baada ya uhusiano na majirani zetu kuimarika, biashara nyingi zaidi zimefanywa katika sekta ya usafiri na kuifanya bandari ya Dar es Salaam kupokea mizigo mingi zaidi katika mwaka huo mmoja pekee.

Dewji alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia, Zambia na nchi zingine jirani ambazo zilikuwa zikitumia bandari za Msumbiji na Afrika Kusini, hivi sasa katika mabadiliko makubwa ambayo yamefanyika kwa kipindi cha mwaka mmoja, zimerudi na kuanza kutumia bandari ya Dar es Salaam kupitisha mizigo yao.

Sambamba na hilo, alimpongeza Rais Samia kwa uamuzi wake mzuri wa kupata mikopo kutoka nje ya nchi, akisema uamuzi huo ni afya sana kwa uchumi wa nchi.

"Ninapongeza uamuzi mzuri wa Rais wa kupata mikopo kutoka nje ya nchi. Hatua hiyo itasaidia uchumi na kutoa ajira nyingi kwa Watanzania wenzetu," alisema.

Mgeni Rasmi katika hafla hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuza Ludigija, alipongeza jitihada zinazofanywa na kampuni za Simba Bingwa na washirika wao kwa jitihada za kutambua na kuthamini mchango wa watumishi wao kwa tuzo na kuhimiza kampuni zingine kujifunza na kuiga mfano huo.

"Kuwatambua wafanyakazi wako kupitia tuzo ni njia bora ya kuonyesha uaminifu kwa wafanyakazi na hii inaweza kuwa mfano mzuri kwa makampuni mengine nchini," alisema.




Mjasiriamali na Mwanamuziki wa Afrojazz, Annette Ngongi (katikati), akiwa na wawakilishi kutoka Konyagi, baada ya kukabidhiwa chupa yenye chapa ya mwanamke mzaramo katika kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Konyagi yazindua chupa kuwakumbuka wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tanzania Distilleries Limited, kupitia kinywaji chake namba moja cha Konyagi, imezindua chupa yenye chapa maalumu, lengo likiwa ni kuwatambua wanawake 50 kwa michango mbalimbali katika jamii.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Meneja wa Chapa ya Konyagi, Pamela Kikuli, alisema kampuni hiyo imezindua zaidi ya chupa 50,000 zenye ujazo wa ml 500 ambazo ni maalumu na zitakuwa na ishara ya mwanamke (mwanamke mzaramo) tofauti na ile yenye ishara ya mwanamume kama ilivyozoeleka. "Kama namna ya kutambua mchango wa wanawake, tumeamua kuzindua chupa hii mpya ambazo itauzwa kwa mwezi huu kwa bei ya Sh. 8,000 ambayo ni bei elekezi," alisema.

Meneja huyo alitoa wito kwa wapenzi wa Konyagi kuwatambua wanawake ambao wamekuwa na michango mbalimbali katika jamii na kuwanunulia chapa hiyo maalumu ikiwa mwendelezo wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika machi 8, mwaka huu, kama namna ya kuwafanya wathaminiwe.

Alisema tayari Konyagi imeshawatambua wanawake 50 ambao wamekuwa na michango mbalimbali katika jamii na wamekabidhiwa chapa hiyo maalumu ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani 2022.

"Chapa hiyo maalumu itapatikana katika maeneo mbalimbali nchini katika mwezi huu na tunatoa wito kwa wateja wetu wachangamkie chapa hii maalumu," alisema meneja huyo huku akiwakumbusha watumiaji wa kinywaji hicho waepuke kunywa na kuendesha vyombo vya moto.

Meneja huyo aliongeza kuwa ishara tu ndiyo itabadilika ila ladha ya Konyagi itabaki vilevile.

"Hatujabadilisha ladha ya Konyagi bali tunawatambua tu wanawake wakati wa Siku ya Wanawake Duniani kwa kuweka ishara ya mwanamke kwa baadhi ya chupa," alisema.

# Safari za treni ndani ya saa 24

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema ujenzi wa daraja jipya la reli ya kati linalojengwa baada ya daraja la zamani kusombwa na maji kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika eneo la kidete, wilayani Kilosa litakamilika ndani ya saa 24 ili kuruhusu huduma za treni kuendelea.

Akizungumza baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi huo jana, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema kurejeshwa kwa safari za treni kutapunguza kero ya usafirishaji wa abiria na mizigo hususani kwa mikoa ya pembezoni mwa Tanzania. "Leo (jana) ni takribani siku ya 10 hakuna bidhaa zinazokwenda mikoa ya pembezoni mwa Tanzania kama Kigoma kwa sababu wanategemea sana reli hii hasa wafanyabiashara. Kukamilika kwa ujenzi huu kutawapunguzia adha wananchi wa maeneo hayo," alisema.

Prof. Mbarawa alilipongeza Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa kufanya uamuzi wa haraka na kuhakikisha huduma zinarejea ndani ya muda mfupi na kuwataka kuzingatia thamani ya fedha zinazotumika nyakati za dharura.

Pia aliupongeza uongozi wa Yapi Markezi kwa kushirikiana kwa karibu na TRC katika kutekeleza ujenzi wa daraja hilo kwa wakati na kwa kuzingatia viwango vilivyokubalika.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alimhakikishia Prof. Mbarawa kuwa shirika linafanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha huduma za usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo zinarejea.

Kadogosa aliongeza kuwa ujenzi wa daraja hilo umegharimu Sh. bilioni tatu na linatarajiwa kukamilika muda wowote kuanzia sasa na hatimaye kuruhusu treni ya majaribio kupita.

Katika hatua nyingine, Prof. Mbarawa aliitaka Wakala wa Barabara (TANROADS) kuangalia upya vipengele vya ujenzi wa mradi wa kiwanda cha Mkulazi ili kujiridhisha na vipengele vilivyopo kama vina tija na vimezingatia uhalisia. Prof. Mbarawa alieleza umuhimu wa kukamilisha mradi huo na kueleza kuwa serikali haitasita kuvunja mkataba na kampuni ya Kay Bouvet Enginerring ya India itakapoona hairidhishwi na maendeleo ya mradi huo. "Hatuwezi kukubali mwende namna hii. Mmeshaandikiwa barua za onyo mbili ikiandikwa ya tatu mkataba utakuwa umeishia hapo sababu hamjatilia uzito na kasi yenu haioneshi kama mtamaliza kwa wakati," alisema.

Mtendaji Mkuu wa Mradi wa Kampuni ya Mkulazi, Selestine Some, alisema mradi huo unapaswa kukamilika Agosti, mwaka huu na kazi zinazoendelea zimefikia zaidi ya asilimia 30.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania tuishangilie Simba inawakilisha taifa

**WAWAKILISHI** pekee wa Tanzania na Ukanda wa Afrika Mashariki waliobakia katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Simba ya jijini Dar es Salaam, kesho watashuka dimbani kukabiliana na RS Berkane kutoka Morocco.

Simba imebakia peke yake katika michuano hiyo ya CAF baada ya Yanga na Azam FC za jijini pia kutolewa mapema sawa na KMKM na JKU kutoka Zanzibar kuaga michuano ya kimataifa kwenye hatua ya awali.

Timu hizo zitakutana katika mchezo wa Kundi D wa michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, wakati mchezo mwingine wa kundi hilo utakuwa ni kati ya ASEC Mimosas ya Ivory Coast dhidi ya US Gendarmerie ya Niger.

Katika msimamo wa kundi hilo, Simba iko katika nafasi ya pili ikiwa na pointi nne sawa na Asec Mimosas wakati vinara ni RS Berkane yenye pointi sita huku US Gendarmerie yenye pointi moja ikiburuza mkia.

Ikiwa nyumbani katika mechi yake ya kwanza dhidi ya ASEC Mimosas, Simba ilipata ushindi wa mabao 3-1 na ililazimisha sare ya ugenini ya bao 1-1, lakini mchezo uliopita ikivaana na RS Berkane huko Morocco ililala kwa magoli 2-0.

Ili Simba ijiweke katika nafasi nzuri ya kusonga mbele, licha ya kubakiwa na mechi mbili mkononi (baada ya kesho), inatakiwa kupata matokeo chanya katika mchezo huo kwa sababu itaongoza kundi hilo au endapo itapata sare basi itaendelea kukaa kwenye nafasi mbili za juu.

Wachezaji wa Simba na benchi la ufundi, huu ni wakati muhimu wa kuongeza umakini katika mechi hiyo ili timu yenu iweze kufikia malengo yake ya kucheza hatua ya nusu fainali au kubeba kombe la michuano hiyo kwa mara ya kwanza.

Hakuna kisichowezekana katika mpira wa miguu, kikubwa ni wachezaji kuongeza utulivu pale wanapokuwa na mpira lakini pia kujipanga kuirudisha kwenye himaya yao wapinzani wanapokuwa wameukamata.

Kama ambavyo walipambana katika mechi ya kwanza, wachezaji wa Simba wanatakiwa kuendelea kujituma kwa sababu ya kusaka ushindi, lakini pia kuendelea kutangaza vipaji vyao kupitia mawakala na makocha kutoka sehemu mbalimbali wanaofuatilia mechi za michuano hiyo.

Kila mchezaji afahamu mechi hiyo inaweza kubadilisha maisha na thamani yake kwa sababu, endapo watapata ushindi au mchezaji ataonyesha kiwango bora, ni wazi watajiweka kwenye nafasi nzuri sokoni.

Tunawakumbusha matokeo mazuri huja pale timu itakapofanya vizuri na maana yake ni wachezaji kupunguza makosa ya kizembe, nyota wa Simba wanatakiwa wafahamu wanakutana na wachezaji wenye uzoefu na michuano hiyo, timu yenye uzoefu na mashindano hayo, moja ya klabu yenye nguvu katika soka la Afrika.

Kama timu kutoka Afrika Magharibi na Kaskazini zimefanikiwa kutawala soka barani, huu ni wakati wa wachezaji walioko Afrika Mashariki kumaliza ubabe wa Waarabu na wao kujitengenezea ufalme mpya kwenye ramani ya mchezo huo unaopendwa na wenye mashabiki wengi zaidi duniani.

Watanzania huu ni wakati muhimu wa kuwa pamoja na Simba kwa sababu ikifanikiwa kusonga mbele, Tanzania itakuwa imepata pointi zaidi ambazo zitasaidia msimu ujao kupata wawakilishi wanne (wawili katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wawili kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika), hivyo tuache itikadi zetu za ndani na kuwa kitu kimoja.


Ujumbe huu pia umekumbushwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla ambaye amewakaribisha mashabiki wa soka kutoka ndani na nje ya jiji hili kujitokeza kuishangilia Simba ili iendelee kuvuna pointi kwenye uwanja wake wa nyumbani.

Kila la kheri Simba, kila la kheri Afrika Mashariki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Nyota Simba, Yanga huumizwa makusudi

**HIVI** karibuni nilimsikia Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameonyesha kusikitishwa na wingi wa majeruhi katika kikosi chake, huku akiwataka waamuzi waochezesha Ligi Kuu Tanzania Bara kulinda wachezaji kutokana na rafu za makusudi zinazofanywa.

Ilikuwa ni baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Nabi alisema waamuzi wa Tanzania wanatakiwa wawe na mamlaka ya kuwalinda wachezaji, si wa Yanga tu, bali wa timu zote ili zisizalishe majeruhi bila sababu yoyote.

Akasema mfano Yanga ina idadi kubwa ya wachezaji majeruhi ambao mara nyingi wanapatikana wakati wa kugongana na wachezaji wa timu pinzani.

"Tunajua ligi ni ngumu na kila timu inahitaji pointi tatu, lakini waamuzi wanatakiwa wawalinde wachezaji na siyo wa Yanga tu, bali hata wa timu nyingine ili zisizalishe majeruhi wengi bila sababu.

Hii si kwa Yanga tu, bali hata Pablo Franco naye amekuwa akilia na tatizo hilo la wachezaji wake kupaniwa na kufanyiwa rafu zisizo za kistaarabu na kimpira.

Ni kweli ukiangalia mpaka sasa klabu kubwa za Simba na Yanga ndizo zina majeruhi wengi kuliko timu zote kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Kuna wakati zilifikisha mpaka majeruhi 10.

Nafikiri kama idadi hiyo ingekua kwa timu zingine ukiondoa hizo, zingekuwa na hali mbaya zaidi kwa sababu huwa hazina vikosi vipana.

Kwa uchunguzi wangu mdogo na mfupi tu, nimegundua timu yoyote ikicheza na Simba na Yanga zinachofanya si kwenda kupambana soka, ufundi na mifumo, bali kwa asilimia kubwa ni matumizi ya nguvu.

Nadhani wamekariri ukicheza na timu hizi ili kuzidhibiti, basi matumizi ya nguvu yanahitajika zaidi. Na wakafanya rafu nyingi ambazo asilimia kubwa ni za kadi nyekundu. Mara nyingi rafu zile kwa sisi tunaotazama soka Ulaya, ni moja kwa moja kadi nyekundu hakuna mjadala.

Kule watu wametoa fedha zao za viingilio na makampuni yamewekeza kwa ajili ya kuona burudani, vipaji vya wachezaji na uwezo, siyo rafu za kipuuzi. Ulaya ukiruka miguu miwili na hata ukimkosa mlengwa unaweza kutolewa nje kwa kadi nyekundu kwa sababu dhamira yako ilikuwa ni kumvunja mwenzako, lakini huku itaangaliwa kama miguu ilimpata au ilimkosa.

Wachezaji wengi wa timu zinazoitwa au kujiita ndogo ukiangalia kwa makini wamekuwa na rafu nyingi za ajabu, si za kistaarabu, za kihusda na kutaka hata kumaliza muda wa wachezaji hao kwa kuwaumiza au kuwavunja.

Hawajali na hawana ile kauli mbiu ya kumlinda mwenzako na wengine wao wanavyocheza ni kama wana visasi nao, au kama wanaowaonea donge kwa sababu wanachezea timu kubwa, hivyo wanataka kuwakomoa.

Wanakuwa na bahati kwa sababu hata wakicheza rafu zao za kupuuzi, si mara nyingi zinarekodiwa na kurudiwarudiwa kwenye mitandao ya kijamii, kama zile ambazo wanacheza wachezaji wa Simba au Yanga.

Bahati mbaya walionayo wachezaji wa Simba au Yanga ambao wanachezewa sana rafu, wao wakirudishia tu video zao zinakuwa zinaonyeshwa sana kwenye mitandao ya kijamii kwa utamaduni ule ule wa U-Simba na U-Yanga kushinikiza wafungiwe, lakini kwa wachezaji wa timu nyingine wanaweza kucheza rafu mbaya sana, lakini isiwe habari ya mjini.

Bahati mbaya zaidi waamuzi nao wametekwa na hilo. Sijui kwa kuwaonea huruma au vipi, wamekuwa wakiwaachia kucheza rafu nyingi bila kuchukua hatua stahiki.

Mchezaji mmoja anaweza kucheza rafu mbaya za kadi nyekundu hata nne, halafu akapata njano moja tu. Na ukiangalia wale wanaopata kadi nyekundu ni wale ambao wana kadi za njano, halafu wanacheza rafu nyingine mbaya. Nadhani waamuzi wanaogopa kuonekana wanazionea timu hizo zinazoitwa ndogo.

Nitakuwa mtu wa mwisho kuamini kuwa Simba na Yanga zina majeruhi wengi kwa sababu ya kutokuwa na mazoezi mazuri ya utimamu wa mwili. Niligundua ni kuchezewa sana rafu mbaya ambazo waamuzi wamekuwa hawachukui hatua stahiki.

# Waziri afagilia ARU kwa utafiti

Na Joseph Mwendapole

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, amekipongeza Chuo Kikuu Ardhi (ARU) kwa kufanya utafiti mbalimbali uliosababisha kupatikana kwa bidhaa ambazo zinaweza kukipatia chuo fedha.

Prof. Mkenda alitoa pongezi hizo jana alipokuwa akifungua mkutano wa kimataifa kuhusu ardhi, mazingira na mabadiliko ya tabia nchi unaoendelea jijini Dar es Salaam.

Alisema chuo hicho kimeweza kuwatumia wasomi wake kufanya utafiti na kuja na bidhaa ambazo iwapo zitafanywa kibiashara zaidi, zinaweza kukiingizia mapato mengi na kuvitaka vyuo vingine kuiga ubunifu kama huo.

"Nakipongeza pia chuo hiki kwa kujenga uhusiano na Shirika la SIDA - Swedeni hali ambayo imewezesha Watanzania watafiti kupata ufadhili wa kufanya utafiti na wengine kwenda kusoma nchini humo," alisema.

Waziri Mkenda alisema kwenye bajeti ijayo, serikali itatenga fedha nyingi kwa ajili ya utafiti na ufadhili wa masomo kwa wanafunzi Watanzania kwenda kusoma fani mbalimbali nje ya nchi.

Alisema pamoja na ukweli kwamba serikali itatenga fedha za utafiti na ufadhili wa wanafunzi, vyuo navyo vinapaswa kujenga uhusiano na vyuo vingine duniani na taasisi mbalimbali kupata miradi mbalimbali.

Alisema Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Evaristo Liwa na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Balozi Salome Sijaona, wamejitahidi kujenga uhusiano mzuri na vyuo mbalimbali duniani.

"Ningependa kuona juhudi zinazofanyika hapa zinafanywa na Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Naambiwa wanafanya juhudi hizi lakini ningependa kuona wanaongeza bidiii," alisema Prof. Mkenda.

Alisema wale mapofesa wanaoweza kuandika maandiko yatakayowashawishi wafadhili kutoa fedha kwa vyuo vyao na kusaidia kuendeleza vyuo hivyo, walindwe badala ya kunyanyaswa.

Prof. Mkenda alisema iliwahi kutokea kwenye mradi mmoja ambao ulikuwa unasomesha Watanzania na kununua makaratasi na mashine za kurudufia lakini watu wakataka kukata kodi kwenye mradi huo.

"Nadhani si sahihi kutoza kodi kwenye vitu vya msaada kwa sababu wenyewe wanaweza kuondoa na hata kupeleka kwenye vyuo vingine kama Makerere na kwingineko ambako hawatozi kodi. Vikwazo vingine tuviondoe ili kuvutia miradi mingi ya msaada kwenye vyuo," alisisitiza.

Alisema maprofesa kwenye vyuo mbalimbali duniani wamekuwa wakiandika miradi mbalimbali ya kuvutia wafadhili na miradi hiyo imekuwa ikipata fedha na kuwa mkombozi mkubwa kwa maendeleo ya vyuo hivyo.

"Vyuo vyote duniani havitegemei fedha za serikali tu bali kupitia miradi inayoandikwa na maprofesa wao. Wanafanya hivyo Afrika Kusini, Misri, Marekani na Sweeden, hivyo hakuna sababu ya Tanzania kushindwa kuandika miradi," alisema.

Kinachotakiwa, alisema ni vyuo kuwawekea mazingira wezeshi ili kutimiza azma yao badala ya kuwawekea vikwazo na hata wanapotaka kusafiri kwenda nje ya nchi waruhusiwe.

Naye Naibu Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Gabriel Kassenga, alisema mkutano huo unashirikisha wadau kuhusu utafiti uliofanywa na ARU kwa kushirikiana na SIDA uliofanywa miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2017.

Alisema mkutano huo unawashirikisha wataalamu wa masuala ya ardhi, mabadiliko ya tabia nchi na mazingira ili kubadilishana mawazo kuhusu matokeo ya utafiti huo yatakavyoboresha sera za ardhi na mabadiliko ya tabia nchi .



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (kushoto), akipokelewa na wanachama wa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), alipowasili kwenye ukumbi wa Mlimani City, mkoani Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kutoa tuzo kwa wanawake waliofanya vizuri kwenye sekta ya viwanda. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kampuni yashinda tuzo sekta ya madini

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya ulinzi ya SGA Tanzania Limited imeibuka mshindi wa tuzo ya mtoa huduma bora zaidi kwa mwaka 2021 katika sekta ya madini na kuzishinda kampuni nyingine zinazotoa huduma hizo kwa mujibu wa sheria ya Madini Sura ya 123.

SGA ilipokea Tuzo na Cheti cha ushindi wakati wa Tamasha la Usiku wa Madini lililoandaliwa na Wizara ya Madini lilofanyika katika Ukumbi wa Mlimani City, ulioko Jijini Dar es Salaam.

Tuzo ya mshindi bora ilitolewa kwa uongozi wa SGA na mgeni rasmi katika hafla hiyo, Rais Mstaafu, Jakaya Kikwete. Tuzo hii ya mwaka huu kwa washiriki wa ndani katika tasnia hii, ni muendelezo wa mafaniko ya utendaji bora unaofanywa na kampuni ya ulinzi ya SGA na ushindi huu unafuatia tuzo nyingine tano za heshima ambazo ilizipata mwaka 2021.

Tamasha la Usiku wa Madini lilihudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta ya madini nchini, ambapo lililenga kuhamasisha wadau wa sekta ya madini na pia kuipongeza serikali kwa mchango wake katika kuboresha sekta ya madini na pia pongezi za serikali kwa kampuni za ndani na nje ya nchi ambayo zinatoa mchango mkubwa katika kukuza sekta ya madini nchini.

Dk. Kikwete alimpongeza Waziri wa Madini, - Dk. Doto Biteko kwa hatua yake ya kuweka mazingira mazuri ya kibiashara ambayo yameongeza fursa za uwekezaji, ambapo alitoa ushauri kwa wizara hiyo kuongeza nguvu ili nchi iendelee kunufaika na rasilimali zake za madini iliyojaliwa kuwa nazo.

SGA ilishinda katika kitengo cha Utendaji wa Maudhui ya Ndani, ambayo mahitaji yake ni pamoja na kampuni iwe imesajiliwa kufanya kazi hapa nchini na asilimia 20 ya umiliki wa hisa zake ziwe zinamilikiwa na Watanzania, ajira ilenge Watanzania kwa asilimia kubwa, aweko Mtanzania kwenye moja wapo ya nafasi za ngazi ya juu za uongozi, mpango mahsusi wa Watanzania kurithi watendaji wanaotoka nje ya nchi, ambapo kigezo kingine ni kuweko kwa programu nzuri katika kuchangia jamii kampuni inapofanyia kazi.

Meneja Mauzo na Masoko wa SGA, Faustina Shoo, alisema kuwa kampuni imepata heshima kubwa kupitia Tuzo hiyo adhimu ya Nafasi ya Kwanza katika utendaji kwa kampuni za ndani na kwamba pia ni heshima kubwa ambayo imepata kutoka Serikalini kupitia Wizara ya Madini.

# Wananchi wakumbushwa kuzingatia kinga UVIKO- 19

Na Sabato Kasika

WAKAZI wa Mkoa wa Dar es Salaam wametakiwa kuzingatia maelekezo ya mwongozo wa Wizara ya Afya kuhusu jinsi ya kujikinga na UVIKO-19 ikiwamo kupata chanjo ili kupunguza kasi ya maambukizi ya ugonjwa huo.

Wito huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, alipozungumzia taarifa ya Mganga Mkuu wa Serikali kuhusu maambukizi ya ugonjwa huo.

"Tumesikia taarifa ya Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, kuhuusu mwenendo wa ugonjwa wa UVIKO-19 nchini, kuwa watu 33,726 wamethibitika kukumbwa nao, huku 800 wakipoteza maisha kwa kipindi cha Machi, mwaka jana hadi Machi 4, mwaka huu," alisema Ngawaiya.

"Katika taarifa yake anasema, idadi hiyo ni kati ya 471,965 sawa na asilimia 7.1 na waliopoteza maisha ni asilimia 2.5 na kwamba kuanzia Februari 5 hadi Machi 4, mwaka huu, kulikuwa na walioripotiwa kupata ugonjwa huo kati ya watu 31,090 waliopimwa na vifo vinane katika mikoa ya Mwanza (vitano), Dodoma (viwili) na Kagera (kimoja)."

Alisema, kilichomshangaza hadi kuamua kuzungumzia suala la UVUKO-19 ni taarifa kuwa kati ya wagonjwa 290, mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa kuwa na wagonjwa 175.

"Hii ni mara ya pili kwa Mkoa wa Dar es Salaam kutajwa kuongoza kwa visa vingi vya ugonjwa, ndiyo maana mimi kama kiongozi wa taasisi ya utawala bora, ninashauri watu wazingatie mwongozo huo," alisema.

Alisema, baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam ni wajuaji hawataki kuzingatia maelekezo ya kujikinga na ugonjwa huo, na kwamba kuanzia mitaani hadi kwenye vyombo vya usafiri, ni kama wamesahau kuwa kuna ugonjwa huo.

Ngawaiya alisema, mwongozo huo unaeleza kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, abiria kutojazana kwenye vyombo vya usafiri, kunawa mikono kwa maji tiririka, kutumia vitakasa mikono na kuvaa barakoa.

"Lakini ukifuatilia utabaini kuwa watu wengi hawazingatii na inawezekana ikawa ni chanzo cha Mkoa wa Dar es Salaam kuongoza kwa maambukizi hayo, hivyo ni vyema taarifa za Mganga Mkuu ziwashtue," alisema.

Alisema, taasisi yake inaunga mkono juhudi zote zinazochukuliwa na serikali za kuwakinga Watanzania dhidii ya ugonjwa, na kwamba anasikitika kuona wakazi wa Dar es Salaam wakiendelea kutochukua hatua sahihi.




Ofisa Muuguzi Msaidizi wa Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Aziza Abdulrahman (wa pili kushoto), akipokea msaada wa vitu mbalimbali zikiwamo sabuni kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu (wa pili kulia), kwa ajili ya kinamama waliojifungua, katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo yalifikia kilele chake, mapema wiki hii. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Chanzo ongezeko saratani watoto chatajwa

**Na Beatrice Shayo**

WATOTO wenye ugonjwa wa saratani wamedaiwa kufikishwa hospitalini wakiwa kwenye hali mbaya kwa ajili ya matibabu, hivyo kuongeza tatizo la ugonjwa huo, imeelezwa.

Kutokana na changamoto hiyo, wazazi wametakiwa kuwawahisha katika vituo vya afya pale wanapoumwa badala ya kuwacheleweshа.

Ofisa Msaidizi wa Shirika la Matumaini la Daisha Tanzania, Lilian Ndyetabula, alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wakipokea msaada kwa ajili ya watoto wenye ugonjwa wa saratani kutoka Kampuni ya Bima ya Reliance, ambao wanapatiwa matibabu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH).

Alisema wazazi hawajui wapi pa kwenda na hali hiyo inasababisha mtoto kufikishwa katika hospitali akiwa katika hatua mbaya na matibabu yake yanakuwa ya gharama na uwezekano wa kupona unapungua.

"Ukiona dadili ya mtoto kuumwa mkimbize kwenye hospitali ya karibu. Usikae naye nyumbani na hasa ukihisi ni ugonjwa wa saratani. Huu ugonjwa unatibika endapo mtoto atawahishwa hospitalini," alisema.

Pia alisema watoto wenye saratani wanakabiliwa na tatizo la kupungukiwa damu, lakini wanashukuru Mungu Muhimbili inatoa kipaumbele kwa watoto wenye saratani.

"Damu inapohitajika kwa watoto hao haijawahi kukosekana. Ningeomba watu ambao wanaweza kuchangia damu kwa ajili ya mtoto mwenye saratani waje Muhimbili kwa sababu damu ni uhai na hawa watoto wanahitaji damu," alisema.

Alisema wamefurahi katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake kutembelewa na wageni wa kampuni ya Reliance ambao wamekuwa ni wadau wao kwa zaidi ya miaka mitano katika kusaidia watoto wenye saratani.

"Wamekuja kujumuika na watoto wetu wenye saratani pamoja na wazazi wao. Kwa kweli wamejisikia faraja uwapo wao umewapa nguvu wazazi hao na kuonyesha kuwa hawako peke yao katika kuwasaidia watoto wao," alisema.

Pia aliwashauri wadau wengine wanapokuwa na chochote wajitahidi kuwakumbuka wahitaji hasa hawa watoto wenye saratani na wazazi wao ambao wanawahudumia.

Alisema saratani ya utotoni inatibika endapo tu mtoto atawahishwa hospitalini na huduma wanazitoa bure, hivyo ni muhimu wazazi kuwawahisha katika vituo vya afya.

Mkuu wa Idara ya Kitengo cha Mawakala na Masoko wa Reliance, Joyce Bendera, alisema wapo katika shughuli za bima kwa miaka 20 na wamekuwa wakitoa huduma ya bima kwa Watanzania.

Alisema waliamua kuitumia Siku ya Wanawake Duniani mahususi kwa ajili ya kwenda kuwaona watoto wenye saratani walioko katika jengo la Ujasiri la MNH.

Bendera alisema watoto hao wametoka katika mikoa mbalimbali hivyo wameona kama wanawake kujumuika nao kurudisha tumaini kwao na kuwapatia furaha.

# Mfumo wa maisha wachangia ukatili dhidi ya watoto

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MFUMO wa utafutaji riziki na wazazi kutowajibika katika malezi ya watoto, vimechangia kuongezeka kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto katika mkoa wa Morogoro.

Kutokana na ongezeko hilo, kituo cha Mkono kwa Mkono kinachohudumia watoto waliokutana na vitendo hivyo, kilichoko Manispaa ya Morogoro, kimewataka wanawake kuwajibika katika malezi ya watoto .

Mratibu wa kituo hicho kilicho chini ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan, Virginia Bamulange, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu nafasi ya mwanamke katika kupambana na vitendo vya ukatili mkoani Morogoro.

Bamulange alisema chanzo cha vitendo vya ukatili kwa watoto wakati mwingine huchanigiwa na kutowajibika kwa jamii husani wanawake katika malezi ya watoto, hivyo kuwataka wazazi na walezi kuanza kuwajibika.

"Ni muhimu sasa wazazi hasa wanawake kuwajibika katika malezi ya watoto,ni lazima ufuatilie mwenendo mzima wa mtoto wako kutokana na mabadiliko ya mfumo wa maisha. Hii itasaidia kudhibiti vitendo vya ukatili kutokea," alisema.

Mratibu huyo pia alitaka jamii na wazazi sasa kuanza kuzungumza na watoto kuhusina na masuala ya uzazi na vitendo vya ukatili kwa uwazi ili wanapokutana navyo waviepuke au kupambana navyo.

Naye Mganga wa Kituo hicho, Dk. Elias Mtungilwa, alisema vitendo vya ukatili kwa watoto vimekuwa vikichangiwa na wazazi au walezi kukimbizana katika kutafuta riziki, hivyo kukosa muda wa kuwa karibu na watoto kujua matatizo yao.

Dk. Mtungilwa alisema mfumo huo wa maisha umechangia kuzuka kwa aina mpya ya ukatili wa watoto kutelekezwa mbali na vitendo vingine vya ukatili kwa watoto ambavyo wamekuwa wakifanyiwa.

Naye Tumaini Kachocho kutoka jamii za kifugaji wilayani Mvomero, alisema bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali za ukatili zikiwamo ndoa na mimba za utotoni. Alisema hali imekuwa kikwazo kwa mtoto wa kike kufikia ndoto zake hasa kielimu.

# Tanzania kurudi uanachama Mahakama ya Afrika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, George Simbachawene, amesema Serikali ya Tanzania ipo katika mchakato wa kurudi kuwa mwanachama wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu baada ya kujitoa kwa muda kutokana na sababu mbalimbali.

Simbachawene, alibainisha hayo juzi baada ya kikao cha pamoja na viongozi wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Katiba na Sheria, Mtumba jijini hapa.

Alisema, suala la Tanzania kujitoa katika Mahakama ya Afrika, zilikuwapo sababu lakini haziwezi kuwa za kudumu.

Waziri Simbachawene alisema kuwa mazungumzo yanaendelea ndani ya serikali na anaamini nchi itarudi tena katika mahakama hiyo.

"Mahakama hii ipo Tanzania, inakuwa si vizuri sana kama tena sisi Watanzania tutakuwa hatupo kwenye hii mahakama tupewe muda, mchakato unaendelea nina imani si muda mrefu maamuzi yatatolewa na serikali," alisema Simbachawene.

Vile vile, alisema Tanzania ni nchi ambayo inatambua, inaheshimu, inatunza na kulinda haki za binadamu na itaendelea kushirikiana na wadau wa masuala ya haki za binadamu.

"Katika mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia ameonyesha nia ya kutunza haki maeneo ambayo yameonyesha kuwa na shida ya haki za binadamu anafanya hivyo kwa vitendo, pamoja na nadharia."

"Wizara ya Katiba na Sheria imefurahi kuona mpo na itaendelea kushirikiana na nanyi katika kila jambo ambalo mtapenda tushirikiane," alisema Simbachawene.

Pia, aliwataka watetezi wa haki za binadamu nchini kuhoji na kuzungumza na wizara, kuliko kupeleka katika majukwaa ya kimataifa na kuiondolea heshima nchi.

Alisema wizara itashiriki kwa pamoja na AZAKI katika majukwaa ya kimataifa ili kuhakikisha Tanzania inajengwa kwa ushirikiano thabiti na wenye tija kati ya pande zote mbili.

Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, katika kikao hicho alitaja baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa maboresho na wizara ikiwamo kuwa na utaratibu mzuri wa kufahamu, kuripoti na kutambua kazi za watetezi wa Haki za Binadamu kama wadau muhimu wa wizara hiyo.

"Pia kufanyika kwa maboresho katika maeneo ya utoaji wa msaada wa kisheria, uboreshwaji wa mifumo ya utoaji haki nchini, maboresho ya baadhi ya sheria ikiwamo sheria ya NGO, hasa katika upatikanaji wa vibali vya tafiti inayoyataka mashirika kupitia TAMISEMI ili kupata pamoja na sheria zingine, ushiriki wa wizara katika mikutano na majukwaa ya kimataifa, Tanzania kurudi katika Mahakama ya Afrika Mashariki," alisema.

Pamoja na maeneo hayo ya maboresho THRDC pia imetoa mapendekezo ya kufanyiwa kazi na wizara katika kuboresha shughuli za utetezi wa haki za binadamu nchini.

Mapendekezo hayo ni pamoja na kuboreshwa kwa mfumo wa utekelezaji (Human Rights Enforcement Mechanism - BRADEA), sheria iliyokuwa inaweka utaratibu wa kulinda haki za kikatiba.

Olengurumwa, alisema mabadiliko yaliyofanyika yameweka vikwazo vingi kwa Mtanzania mmoja mmoja au taaisisi zao kutekeleza agizo la ibara ya 26(2) ya kulinda Katiba.

"Kumekuwa na vigingi vingi ambavyo tunaweza kufanya majadiliano na maboresho kupitia wizara hii ambavyo yatatoa fursa ya Watanzania kwenda moja kwa moja na Taasisi za Haki za Binadamu kwenda mahakamani kulinda na kutetea haki zao kupitia mlango wa kikatiba."





## Chaula ataka haraka mchoro jengo wizara

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula, ametaka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kuharakisha taratibu za kupata mchoro wa jengo la ofisi za wizara hiyo ili ujenzi uanze mapema na kukamilika kwa wakati.

Dk. Chaula alitoa agizo hilo jana alipokuwa akipokea kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za wizara, katika mji wa serikali Mtumba, jijini Dodoma. Wizara hiyo ilianzishwa baada ya kugawanywa iliyokuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Alisema TBA ihakikishe mchakato unakamilika kwa wakati, ili kuiwezesha wizara kuendelea kuhudumia wananchi kwa sababu inagusa makundi yote katika jamii yakiwamo makundi maalumu.

"Kikubwa tunakimbizana na muda kwa hiyo tumeshakabidhiwa eneo hili, hivyo wenzetu wa TBA watoe michoro ili ujenzi uanze kwani wizara hii ni mtambuka" amesema Dk. Chaula.

Mratibu wa Ujenzi wa Mji wa Serikali, Meshack Bandawe, alisema kutokana na mahitaji ya wizara hiyo kwa ukubwa wake, kulikuwa na umuhimu wa kuwa na eneo lake na jengo kamili ili kurahisisha shughuli na kufanya kazi kwa ufanisi zaidi ili kukidhi mahitaji ya serikali kwa miaka ijayo.

"Kwa hatua hii tunatarajia jengo la wizara hii litakuwa miongoni mwa majengo 25 yatakayojengwa hapa Mtumba baada ya taratibu za kimamlaka kukamilika," alisisitiza Bandawe.

Naye Msanifu Majengo wa TBA, Ngh'olo Weja, alisema TBA itatahakikisha mchoro wa majengo hayo unakamilika mapema kwa kufuata sheria pamoja na taratibu zote za kumpata mkandarasi.

# Aweso awa mbogo ucheleweshaji malipo makandarasi miradi ya maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameagiza makandarasi wa miradi ya maji wanaokamilisha kazi wapewe fedha zao kwa wakati badala ya kusumbuliwa kwa kuzifuatilia kwa muda mrefu.

Sambamba na hilo, amewataka watumishi wa sekta ya maji kuacha ubabe na kuwataka kuheshimiana ili malengo ya serikali yafikiwe.

Akizungumza jana kwenye mkutano wa wadau wa sekta ya maji nchini, Aweso alisema tabia ya kuwacheleweshea fedha makandarasi inasababisha kukwamisha utendaji kazi wao.

Pia alisisitiza uaminifu kwa makandarasi huku akitolea mfano mkandarasi wilaya ya Handeni ambaye alilipwa Sh. Milioni 600 lakini hafanyi kazi.

"Alipoulizwa kwa nini hafanyi kazi, mkandarasi huyo alisema ni kwa sababu kuna wachawi, kuna watu wana uwezo wa kufanya kazi lakini wamekuta hawapewi kazi. Haipendezi kupandishana katika makarandinga ya polisi," alisema.

"Pia kuna changamoto kubwa ya baadhi ya makandarasi ni waongo wanapoulizwa kwa nini wamechelewesha kazi, hutoa sababu za uongo," aliongeza.

Aweso alisema kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ametoa Sh. Bilioni 41 kwa ajili ya kulipa makandarasi na kuwataka watendaji wa sekta hiyo kulipa madeni yote wanayodaiwa.

Akichangia kwenye mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA), Mhandisi David Pallangyo, aliwataka wasambazaji wa vifaa vya maji kuweka bei kwenye tovuti zao ili kuwa na uwazi.

"Nasema hivi kwa sababu baadhi ya mamlaka za maji tunajikuta tunatozwa bei zinazotofautiana na wasambazaji wa vifaa wanaofanana,"alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Clement Kivegalo, alisema wako mbioni kutengeneza mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ambao utawezesha makandarasi kujaza vyeti vya malipo (certificate) kwa kutumia mtandao, hivyo kurahisisha utendaji.

Mwakilishi wa makandarasi, Jumanne Werema, alitaja vikwazo vinavyowakabili kuwa ni ucheleweshaji wa misamaha ya kodi la ongezeko la thamani (VAT) na mikataba kutokuwa wazi.



Mbunge wa Mvumi, Livingstone Lusinde (kulia), akijadiliana jambo na wabunge wenzake wa Mkoa wa Dodoma, Waziri wa Uwekezaji ,Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (kushoto) na Mbunge wa Bahi, Keneth Nollo, walipokutana katika Ukumbi wa Msekwa, wakati Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba alipowasilisha mapendekezo ya serikali na mpango wa maendeleo wa taifa wa mwaka 2022/23 na mfumo wa ukomo wa serikali wa bajeti hiyo, Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri Biteko ataja mafanikio sekta ya madini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Dk. Doto Biteko, ameanika mafanikio 12 yaliyopatikana kwenye sekta ya madini kwa kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwamo utoaji wa leseni 8,172 za shughuli za madini.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi kuhusu mafanikio hayo, Dk. Biteko alisema utoaji wa leseni umeongezeka na kwamba kati ya leseni 8,172 zilizotolewa, 5,937 ni za uchimbaji mdogo wa madini, 282 ni za utafutaji wa madini, na tano ni za uchimbaji wa kati wa madini.

Pia alibainisha kwamba leseni mbili kati ya hizo ni za uchimbaji mkubwa wa madini, 49 ni za uchenjuaji wa madini na mbili ni za usafishaji wa madini.

Alisema leseni 1,531 ni za biashara ndogo ya madini na 364 kubwa za biashara ya madini zilitolewa kwa wawekezaji na wananchi, ikilinganishwa na leseni 6,334 zilizotolewa katika kipindi cha kuanzia Machi, 2020 mpaka Februari, mwaka jana.

"Hadi kufikia Desemba, 2021, leseni za uchimbaji mdogo ni 36,400, leseni za utafutaji ni 1,309, leseni za uchimbaji wa kati ni 221, leseni 17 za uchimbaji mkubwa wa madini na leseni 210 za uchenjuaji madini."

"Vile vile, kuna leseni hai sita za usafishaji madini, leseni sita za uyeyushaji madini, leseni 1,649 za biashara ndogo za madini na leseni za 618 za biashara kubwa za madini," alisema. Waziri huyo alisema takribani leseni sita zenye uwekezaji mkubwa na kati zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji miradi hiyo.

"Kwa mara ya kwanza katika historia ya sekta ya madini, serikali ilisaini mikataba mipya minne ya uchimbaji na uanzishwaji wa migodi mikubwa na ya kati ya madini kwa wakati mmoja. Uwekezaji huo una thamani ya dola za Marekani milioni 735.79. Mikataba hiyo ilihusisha uchimbaji wa madini muhimu ya viwandani yanayotokana na mchanga wa baharini, madini ya dhahabu, almasi na madini ya kinywe (graphite), kukamilika kwa mikataba hii ya ubia kati ya serikali na kampuni za madini kunaifanya serikali yetu kunufaika kwa kupitia hisa maalum za asilimia 16."alisema.

Pia alisema kwa kipindi hicho, kiwanda cha kwanza cha kusafisha dhahabu nchini kimezinduliwa cha Mwanza Precious Metals Refinery ambacho kina uwezo wa kusafisha kilo 480 za dhahabu kwa siku kwa kiwango cha kimataifa na ni kikubwa kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Alisema kutokana na ubora wake dhahabu ina uwezo wa kununuliwa na Benki Kuu yoyote duniani na kuwekwa kama amana ya serikali.

"Pia Tume ya Madini kwa sasa inatoa leseni ndogo za biashara ya madini ya ujenzi nay a viwandani ambazo zitachochea na kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye uchimbaji na biashara ya madini na hivyo kuongeza wigo wa ukusanyaji wa maduhuli ya serikali," alisema.





# Waziri avalia njuga mgogoro sugu ardhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, amesema, Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) linahitaji ardhi ya kutosha ili kufanya kazi kwa ufanisi.

Amesema jeshi linahitaji ardhi katika harakati zake ikiwamo eneo kubwa la mazoezi na uhifadhi wa vifaa vya kijeshi, hivyo wananchi walioko katika maeneo yanayopakana na kambi za jeshi, wanapaswa kutoa ushirikiano unaohitajika.

Dk. Tax aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi kijiji cha Kisakasaka kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi wa mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na JWTZ.

Waziri Tax alifanya mkutano huo uliowashirikisha viongozi mbalimbali wa serikali na wananchi wa shehia za Kisakasaka, Maungani na Fuoni ili kumaliza mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu.

"Serikali zetu zote mbili chini ya Rais Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Mwinyi, zimedhamiria kuyatatua matatizo ya ardhi nchini ndiyo maana nimekuja hapa kushuhudia suluhu ya tatizo lililodumu kwa muda mrefu hapa Kisakasaka," alisema.

Tax alisema katika hatua za kumaliza mgogoro huo, wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, zimefanya upimaji na tathmini ya maeneo 83 ya ardhi ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi ili kukamilika kwa wakati.

"Tayari utaratibu umekamilika. Watendaji wako katika hatua za mwisho kuandaa kitabu cha tathmini ili kila mtu apate haki yake," alisema.

Waziri Tax alisema serikali kupitia Bunge la Jamuhuri ya Muungano limetenga fedha kwenye bajeti ya mwaka jana kwa ajili ya kukamilisha malipo ya wananchi walioathiriwa na mgogoro huo.

Mkuu wa Wilaya ya Magharib B, Hamida Mussa Khamis. aliwataka wananchi hao kuiamini serikali kuwa itaendelea kuwalipa fidia kama ilivyoahidi.

Alisema tayari serikali ya Muungano imeshatenga fedha katika hazina yake kwa ajili ya kuwalipa fidia waathiriwa wa mgogoro huo.

Naye Kamishna Msaidizi wa Miliki Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Luteni Kanali Yenu Mgugule, alisema kuchukuliwa kwa baadhi ya maeneo yaliyopakana na kambi za jeshi, kunatokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kijeshi hasa katika zama hizi za sayansi na teknolojia.

Alisema katika upimaji na tathmini, walizingatia zaidi haki za binadamu jambo ambalo litawafanya wananchi wengi wa eneo hilo kushukuru kwa haki zao.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Makazi Zanzibar Joseph Kilangi, aliwaomba wananchi hao kutoa ushirikiano wa kutosha kwa viongozi katika kutatuwa migogoro hiyo. Aidha aliwaomba wananchi hao kutojaribu kujiingiza tena katika maeneo yaliyopatiwa suluhu ili kuepuka matatizo yanayoweza kujitokeza.



Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Lawrence Tax, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kisakasaka, kuhusu utatuzi wa mgogoro wa ardhi uliopo baina yao na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Wilaya ya Magharibi "B", Mkoa wa Mjini Magharibi jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

# SMZ yasema uwajibikaji bado kikwazo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema bado uwajibikaji, uzalendo, kujitolea, kujituma kwa baadhi ya walimu ni changamoto kubwa katika kukuza vipaji na uwezo wa wanafunzi katika shule za serikali na binafsi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, Jamal Kassim Ali, alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa tano wa tathmini ya pamoja ya maendeleo ya sekta ya elimu uliofanyika katika hoteli ya Golden Tulip, Zanzibar.

Alisema hali hiyo inasababisha wadau wengi wa elimu kujiuliza maswali kutokana na wanafunzi wengi kutopata ufaulu mzuri hasa katika mitihani ya taifa.

Pamoja na serikali kuimarisha miundombinu katika sekta hiyo na kutatua changamoto zinazowakabili walimu, alisema bado eneo la uwajibikaji kwa walimu wengi katika maeneo yao ya kazi ni tatizo, hali inayoitia wasiwasi serikali na wadau katika kufikia malengo ya elimu.

Alisema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuzingatia umuhimu wa eneo hilo, imeona kuna haja ya kuliweka bayana suala la uwajibikaji ili wadau kutoa maoni yao na kulipatia ufumbuzi.

Waziri Jamal alisema ni muhimu katika mkutano huo kujadili Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Sheria ya Utumishi wa Umma ya Serikali Namba 2 ya mwaka 2011 ambayo imeweka miundo ya uendeshaji na usimamizi wa utumishi wa umma Zanzibar.

Alisema katika sheria hiyo, kifungu cha 7 (1) kimelezea kanuni za maadili ya utumishi wa umma ikiwamo kila mwajiriwa katika utumishi wa umma kuwajibika kwa kuzingatia mwongozo na kanuni za maadili ya utumishi wa umma na kanuni za maadili ya kitaalamu au fani zilizowekwa maalum kwa ajili ya taaluma au fani fulani.

Jamal alisema serikali bado inahitaji mawazo ya wadau ili kutekeleza mkakati wa kuimarisha uwajibikaji kwa walimu na watendaji katika kada ya ualimu.

"Serikali inatambua mchango wa elimu katika maendeleo ya taifa na katika kukabiliana na ushindani wa kimaendeleo wa kitaifa na kimataifa"alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Khamis Juma, alisema lengo la mkutano huo ni kutathmini kwa pamoja maendeleo ya sekta ya elimu na kutoa maazimio ya utatuzi wa changamoto zinazoikabili, kutafakari na kuweka mikakati maalum.

Mwenyekiti wa Tasisi za Kiraia za Elimu, Salim Ali Salim, aliishauri serikali kuhakikisha mchakato wa wazi wa kupata sera mpya ya elimu inayoenda sambamba na mahitaji ya sasa ya nchi na kielimu.

## Dk. Mwinyi aipongeza Uholanzi kwa misaada

**Na Mwandishi Wetu**

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema utayari wa Uholanzi kuunga mkono mikakati na sera ya uchumi wa buluu, utasaidia kwa kiasi kikubwa kufikia malengo yaliyowekwa.

Dk. Mwinyi alisema hayo Ikulu Zanzibar jana katika mazungumzo kati yake na Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania, Wiebe de Boer.

Katika mazungumzo hayo, Dk. Mwinyi alipongeza azma ya serikali ya Uholanzi kushirikiana na Zanzibar katika kuhakikisha inaimarisha sekta zake za maendeleo ikiwamo uchumi.

Alimweleza Balozi de Boer namna Serikali ya Zanzibar ilivyoweka mikakati yake katika kuimarisha na kuuendeleza uchumi wa buluu huku akitumia fursa hiyo kuwakaribisha wawekezaji kutoka Uholanzi kuwekeza Zanzibar.

Rais Mwinyi alimwahidi Balozi de Boer kwamba serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji watakao amua kuwekeza visiwani hapa.

Naye Balozi de Boer alisema Uholanzi imekuwa na uhusiano mzuri na Tanzania ikiwamo Zanzibar tangu miaka ya 1960 na kusisitiza haja ya kuimarishwa.

De Boer alimwahidi Rais Dk. Mwinyi kwamba Uholanzi iko tayari kuiunga mkono Zanzibar katika kutimiza kiu yake ya kuimarisha uchumi kupitia uchumi wa buluu.

Alisema kwa vile nchi hiyo tayari imepiga hatua kubwa katika sekta za uchumi wa buluu, itahakikisha inaiunga mkono Zanzibar ili nayo ifike pale ilipokusudia ikiwa ni pamoja na kuzishawishi kampuni za nchi hiyo na wawekezaji kuja kuangalia mazingira ya uwekezaji ya Zanzibar.

Pia alisema hatua atakazozichukua katika kuhakikisha anaitangaza vyema Zanzibar kiutalii ikiwamo kuhakikisha yanaandaliwa mazingira mazuri ya usafiri wa watalii kutoka nchi hiyo moja kwa moja hadi Zanzibar kupitia mashirika makubwa ya ndege ya nchi hiyo.



DAYNA NYANGE WAACHE WAJIONEE WENYEWE Uk.13

JUMAMOSI MACHI 12, 2022

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT BURUDANI TELE



## VIDEO YA KUSIKITISHA

# Kuna maswali mengi yanayokosa majibu

SAKATA la kusambaa kwa video ya mwanamuziki Profesa Jay, akionekana yupo katika chumba cha wagonjwa maalum (ICU) limezidi kuleta utata, huku maswali magumu yakiibuka ambayo hayana majibu.

Video hiyo ambayo imeleta ukakasi kwa watu wengi, imesambaa katika mitandao ya kijamii baada ya mtu asiyefahamika kufanikiwa kuingia katika chumba hicho na kuchukua picha.

Hata hivyo, uongozi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), umejitokeza hadharani na kulaani kitendo hicho na kuahidi kumtafuta mtu aliyehusika na kitendo hicho ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano ya Umma, Aminiel Aligaesha, video hiyo ilionekana katika mtandao wa Mange Kimambi, akidai kuwa haikurekodiwa na kusambazwa na hospitali hiyo.

Hata hivyo, baadhi ya watu wamesema kuna maswali mengi kuhusu tukio hilo ambalo uongozi wa hospitali hiyo inatakiwa kujibu wakati wanamtafuta mhusika.

Juma Athumani, amesema uongozi unatakiwa kujibu kuwa mtu huyo alifanikiwa vipi kuingia ndani ya chumba hicho ikiwa kuna mlolongo wa taratibu ambazo zinatakiwa kufuatwa.

"Kuna mambo mengi ambayo unatakiwa kuyatimiza kabla ya kuingia, kwanza mtu anatakiwa kujibu yeye ni nani na kwa nini anakwenda kumuona mgonjwa, Je hili lilitimizwa kabla ya huyo mtu kuingia ndani?" alihoji Athumani.

Pia, ameeleza akikamilisha hapo na kama ameruhusiwa hatakiwi kuingia ndani ya wodi akiwa na vitu vingi, na hata mavazi anavalishwa ya hospitali, kwa hiyo mtu huyo alipewa taratibu hizo?

Swali lingine ni kwamba ndani ya chumba hicho kama mtu sio ndugu wa karibu, hatakiwi kwenda hadi kitandani alipolala mgonjwa na badala yake anamwangalia kwa mbali kupitia kwenye kioo, je huyo mtu ilikuwaje akaruhusiwa kuingia hadi ndani na kufanikiwa kuchukua video bila hofu?

"Jambo lingine ambalo linatakiwa kupata majibu wakati mtu huyo anaruhusiwa kulikuwa na wauguzi wa zamu, kwa nini wasitafutwe na kuulizwa ili kupata majibu sahihi?

Uongozi wa Muhimbili wanatakiwa kujibu maswali hayo ili kuwatosheleza Watanzania ambao wengi wanajiuliza na hakuna majibu kuhusu tukio hilo ambalo limewasikitisha watu wengi.

BASI SAWA

## Ben Pol maisha ya ndoa yana raha yake



MWANAMUZIKI wa miondoko ya taratibu, Ben Pol, amesema hajutii kumuacha mke wake raia wa Kenya, kwani kwa sasa anatamani kurudi tena katika maisha ya ndoa ambayo ameeleza yana raha yake.

Amesema anapenda kuwa na mhimili wa familia, pia anaamini atraingia tena kwenye ndoa hivi karibuni ili kuanzisha familia mpya.

"Maisha hayawezi kwenda kama muhuni au uishi na marafiki kila siku, lazima mtu awe na familia, natamani kuingia tena katika maisha hayo," anesema.

## Nahreel povu la nini kama sio kweli?



PENZI la wanamuziki wa kizazi kipya kati ya mtayarishaji wa muziki, Nahreel na mkewe Aika, imeelezwa limekuwa la muda mrefu, lakini hivi karibuni limeingia doa kutokana na kashfa ya kutoka nje ya ndoa.

Nahreel amekuwa akishtumiwa kupata mtoto nje ya ndoa, lakini mwenyewe amejitokeza akikana akisema hana mtoto mwingine zaidi ya wawili aliopata na mkewe Aika.

Amesema tuhuma hizo hazina ushahidi wowote,hivyo amewaomba watu wenye nia mbaya kucha tabia ya kumpakazia mabaya na kuacha familia yake ikiwa na taharuki.



# Tunda ungeonekana, haya yasingetokea

WAMBEA wa mitandao wamejikuta wakiishiwa pumzi, baada ya Tunda, kueleza wazi kwamba kamwe hawezi kuachana na baba mtoto wake Whozu.

Hivi karibuni kumekuwa na mjadala katika mitandao ya kijamii kuhusu mrembo huyo kuachana na Whozu, kisa muda mwingi hawajaonekana pamoja kama ilivyo kawaida yao.

Tunda amesema Whozu yupo ndani ya moyo wake na kwamba binafsi anampenda na kwamba kile kinachosemwa ni sawa na vichekesho.



# Dayna Nyange waache wajionee wenyewe

MWANAMUZIKI mkongwe wa Bongo Fleva, Dayna Nyange anasema kila mwanamke anapenda kuwa na ngozi nzuri, lakini kutumia madawa ya vipodozi ili kuwa mweupe ni sawa na utumwa.

Dayna Nyange amejibu hivyo kupitia EATV baada ya msanii mwenzake Amber Lulu, kueleza anataka kujichubua ili kuwa mweupe.

Hata hivyo, Nyange anapingana na wazo hilo licha yeye huko nyuma kuwahi kujichubua kwa kutumia vipodozi vikali, lakini kwa sasa hatamani urembo huo.

# Wanawake wa shoka kwenye dansi

Na Adam Fungamwango

KWA sasa kuna akina Zuchu, Nandy, Vanessa Mdee na wengine wengi kwenye muziki wa bongo fleva.

Msingi wao ni wanawake waliokata mnyororo wa kutoruhusiwa kuwa wanamuziki kutokana na mfumo dume ambao kwa sasa unaendelea kupigwa vita duniani kote.

Wazazi wengi huwakaza watoto wao kuwa wanamuziki. Hebu fikiri, watoto wa kiume walikatazwa na waliofanya hivyo wengi wao walitengwa na wazazi wao, kabla ya kurejeshwa kundini baadaye baada ya wazazi kuona mafanikio.

Kwa wanawake ndiyo kabisa, haikufikiriwa. Mwanamuziki wa kwanza kuvunja minyororo hiyo alikuwa ni Tabia Mwanjelwa. Huyu alipigia bendi za Maquiz du Zaire na King Kiki Double O.

Wakafuata kina Nana Njige, Emma Mkelo, Rahma Shally, Asia Daruweshi aliyekuwa akipiga kinanda, Anna Mwaole na wengine wengi.

Kwenye miaka ya mwanzoni mwa 2000, kuliibuka tena wimbi la wanamuziki waimbaji wa kike ambao walitingisha mno tasnia ya muziki wa dansi nchini.

**LUIZA MBUTU**

Ni mwimbaji wa bendi ya African Stars 'Twanga Pepeta', na ana rekodi ya kwamba tangu ajiunge nayo hajawahi kuhama hadi leo hii.

Jina lake halisi ni Luiza Nyoni, jina la Mbutu ni la ukoo wa mumewe, Fariala Mbutu ambaye pia ni mwanamuziki, Fariala ni mtoto wa mpiga solo wa zamani wa Orchestra Makassy, Aimara Mbutu 'Simaro'.

Ametunga na kushiriki kaibia nyimbo zote za Twanga Pepeta ambazo ni nyingi mno na isingewezekana zote kuorodheshwa hapa.

**JESCA CHARLES**

Anaitwa Jesca Charles au 'Jesica Chale.' Huyu alikuwa ni pacha wa Luiza kwenye uimbaji kwenye bendi ya African Stars 'Twanga Pepeta.' Waliimba nyimbo nyingi pamoja. Wakati Luiza akiwa anaendelea na muziki, Jesca kwa sasa ameachana na muziki kwani ameolewa anaishi Ulaya na mumewe.

**HADIJA MNOGA 'KIMOBITEL'**

Ni mmoja ya waimbaji wa kike mwenye sauti 'kavu', ambayo hupendeza sana maskioni mwa msikilizaji kwa mwimbaji wa kike. Huwa haipei sana kama waimbaji wengine wa kike wa kawaida. Ni aina ya sauti za kina 'Miriam Makeba', 'Tshala Muana' au 'Hadija Kopa'. Inawezekana kuwa kitu hicho ndicho kilimfanya awe mwimbaji wa kike aliyeimbia bendi nyingi zaidi maarufu kwa wakati huo kama Twanga Pepeta, African Revolution 'Tamtam', Double M Sound na nyingine nyingi.

Jina la Kimobitel alipewa na mashabiki wake kutokana na umbile lake dogo na wembamba, akifananishwa na simu za wakati ule, ambazo 'eti' zilionekana ni ndogo.

**AMINA NGALUMA**

Alikuwa mmoja wa wanamuziki mahiri wa kike. Unaweza kumsikia vizuri kwenye wimbo wa 'Mgumba' namba mbili, alivyolalamika. Ule namba moja uliimbwa na Hadija Kimobitel.

Alifariki dunia akiwa nchini Thailand mwaka 2014. Mwimbaji huyo aliyepachikwa jina la 'Japanese', alipitia bendi za Twanga Pepeta, Double M Sound, 'Tamtam' na TOT Plus.

**NYOTA KINGUTI**

Anaitwa Nyota Kinguti kabla ya kuwa Nyota Waziri alipoolewa na Waziri Ally. Ni dada wa mwanamuziki maarufu nchini Ramadhani Kinguti anayetokea kwenye ukoo wa muziki, kwani kaka yao Adam Kinguti ndiye alikuwa mmiliki wa bendi ya Bicco Stars. Naye alitokea kwenye bendi hiyo hiyo, lakini alikwenda Kilimanjaro Band 'Wana Njenje' baada ya kuolewa na Waziri ambaye kwa sasa ni marehemu. Ameimba nyimbo nyingi kama 'Tulizana Mpenzi', 'Gere' na nyingine. Kwa sasa hasikiki sana kama ilivyokuwa hapo awali.






# Kijiti; Mfalme mwenye akili kisoda

Na Adam Fungamwango

HAKUNA kilichoamriwa na Mungu duniani, mwanadamu akakipinga na akabaki kuwa salama. Alimwambia Adam kule bustanini kuwa utakula kwa jasho, na chakula chako kitakuwa ni mboga za makondeni, na vyote vitatoka ardhini.

Ndiyo, hadi leo hakuna chakula cha binadamu kinatoka juu. Vinatoka ardhini kwa sababu vinalimwa. Binadamu hawezi kula kitu chochote ambacho hakikutoka chini ya ardhi akabaki hai.

Mungu alisema mkazaane mkaijaze dunia. Alimwambia Adam, naye akawaambia wanae na wajukuu zake. Hadi leo hii mtaji wa nguvu ya dunia na nchi zote ni watu.

Taifa lisilo la watu ambao ndiyo nguvu kazi ni taifa mfu. Akitoka mtu akasema msizaane, basi ana matatizo kichwani.

Kwenye filamu hii ya Kijiti, tunakutana na mfalme Msisiri wa Msisiri wa himaya ya Tetete aliyeamuru watu wote wa himaya yake waache kuzaliana kwa miaka saba kwa sababu wanamaliza ardhi. Wanakosa ardhi ya kulima. Akaitisha kikao na kuamuru hilo. Yoyote ambaye atapinga, adhabu yake ilikuwa ni kifo.

"Tunakosa ardhi ya kulima na kelele moja kwa moja. Naamini baada ya miaka saba tutakuwa tumepungua na watu waanze kuzaa."

Akaamuru.

Akaongeza na mfumo dume. Ni kwamba wanawake hawazai bila mwanaume. Lakini adhabu ikaonekana kuwalenga wanawake wanaopata ujauzito kuuawa na si wanaume waliowapa.

Walioanza kupinga, wengine walionywa na wapo waliouawa. Pamoja na sheria hiyo mbovu, baadhi ya wanawake walianza kupata ujauzito, wakapata adhabu hiyo, na hata waliojaribu kutoroka walikamatwa na wote waliuawa hadharani ili kuwatisha wengine. Hali ilizidi kuwa mbaya, ni mauaji na vilio tu kwenye himaya ya Tetete.

Siku ikafika binti mfalme naye akapata ujauzito. Lilikuwa kama pigo kwa mfalme, kwani sasa hakujua la kufanya. Alichofanya alirekebisha sheria yake, badala ya kumuua binti yake, sasa adhabu ikahamia kwa aliyempa mimba ambaye ni Kijiti, kijana mmoja kijijini hapo. Kijiti alipouawa, Kibena binti mfalme naye alijinyonga.

Ilikuwa ni huzuni kuu kwa mfalme. Akaanza kuwa mgonjwa. Mzimu wa kike ukatokea kwenye himaya hiyo na kuanza waua wote walioshirikiana na mfalme, hatimaye mfalme mwenyewe akauawa.

Mzimu huo ukamkabidhi madaraka mtoto wa mfalme Simbira, lakini ukimtaka asitawale kikatili kama baba yake.



# Timaya kumbe na wewe mwoga?

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Timaya, ameondoa ukimya baada ya kujitokeza na kueleza kukamatwa kwake na polisi kutokana na kitendo chake cha kukimbia baada ya kusababisha ajali.

Mwanzoni mwa mwezi huu, mtumiaji mmoja wa mtandao wa Instagram, Osinubi Omowumi, alilalamika kuwa msanii huyo alisababisha kifo cha dada yake.

Kulingana na Timaya, baada ya kumgonga binti huyo kwa bahati mbaya, aliogopa baada ya wanaume wawili kumvamia na kumtishia kumdhuru.



## Kim acha hasira jamani

STAA wa kipindi cha maisha ya kila siku wa Marekani, Kim Kardashian, ameamua kumfuta aliyekuwa mume wake Kanye West, katika orodha ya wafuasi wake katika mtandao wa Instagram.

Mama huyo wa watoto wanne, alichukua uamuzi huo mara baada ya mahakama ya Los Angeles, kuthibitisha kwamba yuko huru kutumia jina lake baada ya ndoa yao kuvunjika.

Kim alithibitisha kuwa yupo singo mbele ya Jaji Steve Cochran, baada ya ndoa hiyo kushindikana kusuluhishwa kutokana na wawili hao kuwa na wapenzi tofauti.

## Baba Ijesha aanza kujitetea


MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Olarewaju James, maarufu kama Baba Ijesha, ameanza kutoa ushahidi mbele ya Mahakama ya Makosa Maalum ya Ikeja, kwa kueleza alikuwa akiweka maandishi kwenye video ya mtandaoni na binti ambaye anatuhumiwa kumbaka.

Shirika la Habari la Nigeria (NAN) limeripoti kuwa Baba Ijesha, amefichua hayo alipokuwa akijetetea huku akiongozwa na wakili wa utetezi.

Baba Ijesha aliiambia mahakama kuwa mama mlezi wa mtoto huyo Bi Damilola Adekoya ambaye ni msanii wa vichekesho, anayejulikana kama Princess, alimpigia simu na kumtaka awe sehemu ya utayarishaji wa filamu hiyo.

" Princess alinitumia ujumbe kwamba alitaka kuanza uzalishaji na angependa niigize nafasi ya mvulana ambapo nilimjibu sawa" amesema.





## Mazito yaibuka kesi ya Chris Brown

MAMBO mapya yameibuka kuhusu madai ya ubakaji yanayomkabili mwanamuziki wa Marekani, Chris Brown. Katika taarifa zilizopatikana hivi karibuni, zinaeleza Mwanamke Jane Doe, ambaye alimshutumu nyota huyo wa muziki kwa kumbaka nje ya nyumba ya P Diddy, mwaka 2020, zinaonyesha sio za kweli.

Kulingana na ujumbe mfupi wa maneno walionasa polisi wa Miami, zinatoa picha kwamba wawili hao walikuwa wapenzi na hakukuwa na dalili ya ubakaji.

Jumbe hizo pia zilifichua jinsi Doe alivyokuwa akimsifia Brown kuwa anajua mapenzi na alijibiwa na nyota huyo kuwa afanye kila iwezekanavyo asipate ujauzito kwani wanashiriki bila kinga.

## Kanye West bado hujafika?

RAPA wa Marekani, Kanye West, amesema mpenzi wake mpya Chaney Jones, ana asili ya kizungu na Kiafrika.

Mrembo huyo ambaye kimwonekano anafanana na mke wake wa zamani Kim Kardashian, amekuwa gumzo kutokana na watu kutojua asili yake kama ni mzungu au mweusi.

Hata hivyo, Jones mwenyewe kupitia akaunti yake ya Instagram, amekiri kwamba yeye ni mchanganyiko wa wazazi wake kutoka Ulaya na Afrika magharibi katika nchi ya Nigeria.



MAKALA

# Tanzania inapojizatiti kuongoza mifugo,uvuvi

## ●Mauzo ya nyama yapaa asilimia 200
## ●Kujenga bandari kubwa ya uvuvi Kilwa

**Na Moshi Lusonzo**

TANZANIA ni moja ya nchi inayoongoza kuwa na utajiri wa mifugo na viumbe maji katika bara la Afrika, lakini kwa miaka mingi imekuwa nyuma kuitumia kama chanzo muhimu cha pato la Taifa.

Hata hivyo, serikali ya awamu ya sita imeamua kwa makusudi kuinua sekta hizo na kuiwezesha nchi kuwa kinara wa uuzaji nyama nje na samaki katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Akitoa tathimini ya wizara yake ya mwaka mmoja tangu Rais Samia Suluhu Hassan, aingie madarakani, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, anasema mikakati inafanyika kwa kasi kufikia kiwango hicho na tayari mafanikio yameanza kupatikana.

Anasema ndani ya kipindi hicho, wizara yake imefanikiwa kuongeza kasi ya usafirishaji wa nyama na ngozi nje baada ya kutafuta masoko ya uhakika katika nchi za Asia na Mashariki ya Kati.

Waziri Ndaki, anasema uuzaji nyama nje ya nchi umefikia kiasi cha tani 5,340 sawa na zaidi ya asilimia 200 katika kipindi cha nusu mwaka, kutoka tani 1,774.29 zilizouzwa mwaka jana.

Anasema mauzo hayo ni kuanzia mwezi Julai, 2021 mpaka Januari mwaka huu, serikali imeingiza dola milioni 22.4, sawa na shilingi bilioni 52.1, kutoka 9.9 zilizopatikana mwaka uliopita.

Anaeleza kutokana na kazi kubwa ya Rais Samia Suluhu Hassan, Tanzania imefanikiwa kupata soko la nyama katika nchi za Oman, Kuwait, Qatar, Saudi Arabia na Hong Kong.

Saudi Arabia pekee wao wanahitaji tani 700,000 kwa mwaka na tayari wataalamu kutoka nchi hiyo wamekuja nchini kukagua baadhi ya viwanda vya kuchinja na kuchakata nyama na wameridhika.

**MAFANIKIO SEKTA YA MIFUGO**

Mafanikio mengi yamepatika katika Serikali ya Awamu ya sita kupitia sekta ya mifugo, moja ya mafanikio hayo ni udhibiti wa magonjwa ya mifugo na upatikanaji wa chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo.

Waziri Ndaki, anaeleza serikali inaendelea kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kuzalisha chanjo ya magonjwa ya kipaumbele ambapo dozi 128,146,275 zimezalishwa kupitia taasisi ya chanjo (TVI) pamoja na sekta binafsi.

Katika mkakati huo wa chanjo, Serikali imeimarisha taasisi ya chanjo kwa kuipatia mashine na vifaa vya thamani ya shilingi 2,400,000,000, huku Kampuni binafsi ya NOVABI ikizalisha dozi 50,000,000 za chanjo aina ya tatu moja dhidi ya ugonjwa wa mdondo, ndui na mafua ya kuku.

Uwekezaji wa sekta binafsi pia umesaidia ongezeko la uzalishaji wa chanjo hapa nchini, kampuni ya Hester Bioscience Africa Limited katika kipindi cha mwaka mmoja imezalisha dozi 6,130,000 ya magonjwa ya CBPP, PPR, mdondo na Gumboro.

Kuhusu udhibiti wa magonjwa kwa njia ya uogeshaji, serikali imenunua lita 33,759 za dawa za kuogesha mifugo kwa shilingi bilioni 1.3 na kuwezesha wastani wa michovyo 462,167,216 kwa ng'ombe 289,097,367, mbuzi 198,958,720 na kondoo 111,943,913.

"Serikali imeimarisha udhibiti wa magonjwa yaenezwayo na kupe na wadudu wengine kwa kuwezesha ujenzi wa majosho mapya 230 na ukarabati wa majosho 80 kwa zaidi ya shilingi bilioni 3.9," anasema Waziri Ndaki.

Aidha, katika kuhakikisha shughuli za sekta ya mifugo zinaenda vyema Serikali imeboresha shughuli za ugani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kununua pikipiki 300 na kuzigawa katika halmashauri.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki

**BIDHAA ZA NGOZI, MAZIWA ZAIMARIKA**

Waziri Ndaki, anasema bidhaa za ngozi za wanyama zimeendelea kuimarisha sekta binafsi na kuwezesha uzalishaji wa viatu vya ngozi jozi 3,004,700, huku jumla ya vipande 73,607 vyenye thamani ya shilingi 460,043,750 viliuzwa nje ya nchi.

Kwa upande wa maziwa, serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imewezesha uwepo wa vituo 238 vya kukusanyia na kupooza maziwa, huku viwanda vya kusindika maziwa vimefikia 104 na kufanya uzalishaji wa maziwa kuongezeka kwa asilimia 12.1, kutoka lita bilioni 2.7 hadi 3.1.

Katika kuweka mfumo imara wa utambuzi wa mifugo yote nchini, serikali imeanza kuwatambua kwa kutumia elektroniki na mpaka kufikia Januari mwaka huu, jumla ya mifugo 1,504,659 katika mikoa 14 imewekwa hereni za kielektroniki.

Katika utambuzi huo ng'ombe wapo 1,219,481, mbuzi 167,298, kondoo 61,571 na punda 56,309.

**SEKTA YA UVUVI YAPAA**

Waziri huyo anaeleza kwamba sekta ya Uvuvi imezidi kupaa na kuifanya kuwa moja ya muhimili wa kutoa ajira na lishe bora kwa jamii hapa nchini.

Anaeleza mpaka sasa sekta hiyo inachangia uhakika wa upatikanaji wa chakula na lishe kwa asilimia 30, na ajira 195,435 za uvuvi na milioni 4.5 za wafanyabiashara wa mazao ya majini.

Miradi hiyo imejikita kulinda rasilimali za uvuvi, kukuza sekta binafsi kupitia uwekezaji, kujengea uwezo jamii ya wavuvi, kuboresha mazao ya uvuvi, miundombinu ya uvuvi, kufanya utafiti na kuboresha mfumo wa taarifa za uvuvi.

Ndaki anasema katika kuimarisha shughuli ya uvuvi na kuwa moja ya nchi inayoongoza kwa uuzaji wa samaki, tayari serikali imetangaza tenda kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi itakayojengwa eneo la Kilwa.

"Serikali imetangaza tenda kwa ajili ya ujenzi wa bandari hii kubwa, tunataka kuona Tanzania inakuwa nchi pekee inayosambaza samaki katika ukanda wetu, na hili litafanikiwa ndani ya miaka michache," anaongeza kusema.

Anasema mradi mwingine unaotekelezwa ni Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi(SWIOFish) ambao unalenga kuongeza faida za kiuchumi, kijamii na kimazingira katika mwambao wa Bahari na ukanda wa Uchumi wa Bahari.

Mradi ho una thamani ya Dola Milioni 36 ambapo Tanzania Bara ilipata Dola milioni 17.28, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dola milioni 11.52 na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) Dola milioni 7.2.

Pia katika kipindi hicho uimarishwaji umefanyika wa miundombinu ya uvuvi ikiwemo Maabara ya Utafiti wa Uvuvi mkoa wa Dar es Salaam, nyumba tatu za watumishi mkoani Tanga (TACMP) na ofisi tano.

SErikali pia itatumia bilioni 20 kwa kununua Meli nne za Uvuvi kwa upande wa Tanzania Bara.

"Tumejidhatiti katika ukuzaji wa viumbe maji kwa kujenga vituo vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji ikiwemo Ujenzi wa kituo Rubambagwe, kilichopo katika Mkoa wa Geita na kugharimu zaidi ya bilioni tatu. Utanuzi wa kituo cha Ruhila kitakachotumia milioni 202," anasema Waziri Ndaki.

Kutokana na kuweka sheria na Kanuni rafiki zimechochea uwekezaji katika uvuvi na kuipatia serikali zote mbili asilimia 50 ya mapato kama gawio.



Ng'ombe waliotambuliwa na kuvalishwa hereni za kielektroniki

TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOELEKEA...

# Unakikumbuka kivuko cha utete? Mrithi Daraja Mkapa aliyeacha vilio

**Na Adam Fungamwango**




YOYOTE aliyekuwa nje ya nchi kwa miaka mingi na alikuwa hafuatilii chochote kilichopo nchini, akarejea, ukimwambia kuwa unakwenda mkoani Lindi na Mtwara na utafika leo hii hii, anaweza kukushangaa na kuishia kucheka.

Ndiyo, kwa sababu atakumbuka kuwa ili kutoka mikoa hiyo ya Kusini kufika Dar, au kutoka Dar kwenda huko, ilikuwa safari ambayo kama ukiwahi sana inaweza kuwa ni siku tatu au nne.

Kama si hivyo inaweza ikawa ya wiki, wakati mwingine mwezi mzima. Unaweza kumuuliza sababu, akakwambia ukifika Rufiji ni lazima usubiri kivuko, au utumie usafiri wa hatari zaidi wa kuvuka na ngalawa au mtumbwi.

Utamshangaza zaidi ukimwambia kuwa kwa sasa kuna daraja. Nadhani atakuuliza maswali kadhaa ili kuthibitisha hicho unachokisema.

Daraja la Mkapa lilifunguliwa rasmi Agosti 2, 2003 na Rais wa awamu ya tatu wakati huo, Benjamin Mkapa ambaye ndiye aliyekuwa chachu ya kujengwa, na awali ilionekana ni kama ndoto hivi.

Daraja hilo lenye urefu wa mita 970 ambalo limeunganisha mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara, lililopo Ikwiriri mkoani Pwani, limekuwa ndiyo mkombozi siyo tu kwenye usafiri, lakini kumaliza mateso, visa, mikasa na vifo vya wananchi wengi waliokuwa wakipoteza maisha kwa sababu mbalimbali, lakini kikubwa ikiwa ni uhaba wa kivuko.

Rais Mkapa na viongozi wenzake wanaona hakukuwa na haja ya kununua vivuko vingi kama Feri la Kigamboni, bali kujengwa daraja.

Ndiyo daraja refu zaidi kuliko yote Tanzania mpaka sasa na daraja la tisa kwa urefu Afrika.

Kivuko kikuukuu kilichokuwepo hapo kilitesa sana watu, hususan abiria, kwani mbali na ubovu wake, lakini pia kilishindwa kumudu wingi wa abiria wanaotoka Dar kwenda Kusini na wanaotoka Kusini na kwenda Dar.

Inabidi abiria wasubiri wanaovuka upande mmoja na mabasi yao, na upande mwingine na mabasi yao, kwa utaratibu maalum ili kukifanya kisizidishe abiria na mizigo.

Hii ilifanya watu waishi sehemu hiyo kwa siku moja, mbili tatu na kuendelea kutegemea abiria waliopo.

Mbaya zaidi usiombe pantoni ya MV Utete iharibike. Ni hatari zaidi ya hatari yenyewe, kwani baadhi walikuwa wakivuka na mitumbwi midogo, ambayo wakati mwingine ilikuwa inashindwa kumudu kubeba abiria na kupinduka.

Hapo ndipo vifo vingi vilikuwa vinatokea kwa abiria kuwa chakula cha mamba na kuuawa na viboko wanaotapakaa kwenye mto huo.

Nakumbuka mwishoni mwa miaka ya 1970, nikiwa mdogo, mpangaji wenzetu mmoja alipata safari ya kwenda kwao Lindi akiwa na mke na watoto wanne.

Tulishangaa aliporejea akiwa na mtoto mmoja tu. Tulipouliza kama wamebaki walikokwenda, tukaambiwa japo kwa lugha ya kuambiwa sisi watoto kuwa wamezama kwenye mto Rufiji baada ya mtumbwi waliokuwa wakivuka kupinduka. Waliobaki ni mwenyewe baba, mke na mtoto mmoja wa kwanza. Watatu wote waliishia mto Rufiji. Kisa ni kwamba walipofika walikuta kivuko ni kibovu na haikujulikana lini. Baadhi ya abiria wenye pesa au haraka waliamua kukodi mitumbwi kwa malipo ili kuwahi, na wasiokuwa nazo walipata adha ya kukaa wakati mwingine kwa muda mrefu, njaa, mbu, na mateso kibao vikiwakabili.




Mmoja wa Wahandisi waliosimamia ujezi wa daraja la Mkapa, Mhandisi Kaitanda Michael aliwahi kubainisha na kuainisha mateso waliopitia si abiria tu, bali hata wananchi wa maeneo hayo kabla ya daraja hilo kujengwa ni pamoja na kushindwa kuvuka Mto Rufiji kwenda ng'ambo ya pili kufuata huduma kutokana na mto huo kujaa maji pamoja na mamba wengi hususan wakati wa masika.



"Mara kadhaa kivuko kilikwama kwenye matope kwa siku zisizotabirika na kusababisha msongamano mkubwa wa magari, wanafunzi walitaabika kwa kukosa chakula kwa siku kadhaa na hawakujua lini watanasuliwa na kuweza kuendelea na safari. Changamoto haikuwa hiyo pekee, akina mama wajawazito waliteseka kwa kusoka huduma za uzazi, wapo waliojifungua njiani, wengine walipoteza maisha yao na ya watoto, hata vitendo vya ukatili wa kijinsia vilikuwa vinafanyika." Alisema Mhandishi huyo na kuongeza

"Kutokana na kukosekana kwa miundombinu imara hususan daraja na barabara, suala la usafiri na usafirishaji wa bidhaa katika mikoa hiyo ya kusini ilighubikwa na changamoto lukuki na hivyo kusababisha gharama za maisha kuwa juu ambapo bidhaa kama sukari ilipanda mara tano ya bei iliyokuwepo wakati huo. Hapakuwa na watu wenye maono ya shughuli za kiuchumi kwa sababu ya kukosa mawasiliano, hakuna masoko, Mfanyakazi wa serikali akipata uhamisho kwenda mikoa ya kusini utasikia watu wakiuliza amekosa nini, ilikiwa ni kama adhabu." Alisema.

Rufiji ni mto mkubwa wa Tanzania, chanzo chake kikiwa ni Kusini Magharibi ya nchi, kwenye maungano ya matawi la mto Kilombero na Luwegu. Matawi ya mito hiyo, huungana na kuunda mto Rufiji ambao unaanza safari yake ya unatiririsha maji na kuishia kwenye Bahari ya Hindi.

**Tuma meseji 0716 350534**

# Putin aomba msaada kuipiga Ukraine



Mwanajeshi wa Ukraine akimfariji mwanamke anayelia kutokana na mashambulizi ya anga yanayoendelea kufanywa na vikosi vya Russia**: PICHA BBC**

RAIS wa Russia Vladimir Putin, inadaiwa ametoa ruhusa kuhusu mipango ya kutuma wapiganaji wa kujitolea nchini Ukraine.

Kulingana na ripoti moja, ilieleza Rais Putin, alizungumza katika mkutano wa baraza la usalama la Taifa, kuwa watu kutoka nje ya nchi hiyo wanaotaka kujitolea kupigana na vikosi vinavyoungwa mkono na Russia wanapaswa kuruhusiwa.

Waziri wa Ulinzi wa nchi hiyo, Sergei Shoigu, alisema kuna watu 16,000 wa kujitolea katika nchi za Mashariki ya Kati ambao walikuwa tayari kwenda kupigana na vikosi vinavyoungwa mkono na Russia, shirika la habari la Reuters linaripoti.

Wakati huo huo, vikosi vya Russia vimewauwa raia wengi wa Ukraine kuliko wanajeshi katika wiki mbili tangu uvamizi huo uanze.

Waziri wa Ulinzi wa Ukraine, Oleksii Reznikov, alisema "Nataka hii isikike sio tu huko Kyiv, lakini ulimwenguni kote," Maoni yake yanakuja huku vikosi vya Russia vikionekana kupanua mashambulizi yao dhidi ya nchi hiyo na kuanzisha mashambulizi katika miji mingine pande tofauti za nchi.

PICHA za satelaiti zilizopigwa na kampuni moja ya Marekani zinaonyesha msafara mkubwa wa kijeshi wa Russia karibu na mji mkuu wa Ukraine, Kyiv.

Imeelezwa msafara huo umetumwa mara ya pili na ulionekana kuwa na umbali mrefu.

Msafara huo ulionekana mara ya mwisho karibu na Uwanja wa Ndege wa Antonov, kaskazini magharibi mwa mji wa Kyiv, na mwenendo wake unaweza kuashiria kuelekea mjini humo.

Kampuni iliyopiga picha hizo, Maxar Technologies, ilisema sehemu ya msafara huo ilikuwa katika maeneo ya miji jirani.

Sehemu zingine ziko kaskazini zaidi, na makombora yakiwa katika mkao wa kuwa tayari kurushwa.

Upelekaji huo upya wa zana hizo za kivita unawadia wakati vikosi vya Russia vilianza kushambulia maeneo mapya yaliyolengwa katika maeneo tofauti ya Ukraine.

Katika mashambulizi hayo mapya, uwanja wa ndege na kiwanda cha injini ya ndege vimelengwa huko Lutsk, kaskazini-magharibi na kisha milipuko ilipiga viwanja vya ndege huko Ivano-Frankivsk, kusini-magharibi.

Kwa upande wa Dnipro, ngome kuu mashariki mwa Ukraine, ilishambuliwa na mtu mmoja ameripotiwa kufariki dunia.

### FACEBOOK KURUHUSU WITO WA GHASIA

Mmiliki wa Facebook na Instagram ataruhusu watumiaji katika baadhi ya nchi kuitisha ghasia dhidi ya Rais Vladimir Putin na wanajeshi wa Russia.

Meta ilisema imetoa ruhusa kwa muda kwa baadhi ya matamshi ya vurugu, kama "kifo kwa wavamizi wa Urusi," ambayo kwa kawaida inaweza kuvunja sheria za mtandao huo.

Hata hivyo, ilisema haitaruhusu wito wa vurugu dhidi ya raia wa Urusi.

Kujibu tamko hilo, Russia iliitaka Marekani kusitisha shughuli za itikadi kali katika mtandao huo wa kijamii.

Tangazo hilo lilikuja baada ya shirika la habari la Reuters, kusema kuwa limeona barua pepe za ndani zinazoelezea mabadiliko hayo ya sera.

"Kwa kuzingatia uvamizi unaoendelea wa Ukraine tuliweka ubaguzi wa muda kwa wale walioathiriwa na vita, kuelezea hisia kali dhidi ya vikosi vinavyovamia," msemaji wa Meta aliiambia BBC.

Chini ya sera hiyo iliyofanyiwa marekebisho, watumiaji katika nchi zikiwemo Russia, Ukraine na Poland pia wataweza kutoa wito wa kuuawa kwa Rais Putin wa Russia na Rais wa Belarus Lukashenko.

Barua pepe hizo zinaripotiwa kusema wito wa vifo vya viongozi hao utaruhusiwa isipokuwa kama zitakuwa na malengo mengine, au kujumuisha eneo au mbinu.

Wito wa unyanyasaji dhidi ya Warussia pia unaruhusiwa wakati chapisho linaweka wazi uvamizi wa Ukraine, barua pepe ziliripotiwa kusema

"Tunazitaka mamlaka za Marekani kusitisha shughuli za itikadi kali za Meta, kuchukua hatua za kuwafikisha wahusika kwenye vyombo vya sheria," ubalozi wa Russia nchini Marekani ulisema kupitia Twitter.

Ubalozi huo uliongeza "Watumiaji wa Facebook na Instagram hawakuwapa wamiliki wa majukwaa haya haki ya kuamua vigezo vya ukweli na kugombanisha mataifa dhidi ya kila mmoja," iliongeza.

### MASHAMBULIZI YANASONGA MAGHARIBI

Mashambulizi ya anga yamesikika katika miji ya magharibi ya Lutsk na Ivano-Frankivsk jana asubuhi.

Pia vikosi vya anga vya Russia vimeshambulia ngome iliyoko eneo la kati ya magharibi ya Dnipro kwa mara ya kwanza tangu uvamizi huo uanze zaidi ya wiki mbili zilizopita.

Wakimbizi kutoka miji iliyokumbwa na mashambulizi ya mabomu walikimbilia magharibi mwa Ukraine wakiamini kuwa ni salama zaidi.

Maelfu ya watu walipitia mji wa Lviv, kitovu kikubwa cha raia kupumzikia.

Mashambulizi ya jana yalilenga miji iliyoko pande zote mbili.

Meya wa Ivano-Frankivsk, alithibitisha kushambuliwa kwa makombora katika mji wake kusini-magharibi mwa Ukraine.

Katika ujumbe wa Facebook, alisema "Adui alimpiga Frankivsk."

Aliwataka watu kutoshiriki picha na video za milipuko hiyo na alionekana kupendekeza mfumo wa kengele wa mgomo wa makombora ufanyike.

Aliwaonya wakazi wa wilaya za Krykhivtsi, Chukalovka, Opryshivtsi, Gorodok kutotoka majumbani

"Kaa nyumbani kwa usalama wako! Wakati hatari itapita - nitakufahamisha," aliongeza.

Vikosi vinavyoungwa mkono na Russia vilikamata Volnovakha, ripoti zinasema

Huku mashambulizi mapya yakiripotiwa kote Ukraine, sasa kuna ripoti kwamba watu wanaotaka kujitenga wanaoungwa mkono na Russia wameuteka mji muhimu wa kimkakati wa Volnovakha, kaskazini mwa bandari iliyozingirwa ya Mariupol, shirika la habari la RIA limenukuu wizara ya ulinzi ya Russia.

### MAJESHI YA RUSSIA YAIZINGIRA KYIV

Picha za satelaiti zilionyesha msafara wa Russia umeuzingira mji wa Kyiv, na kuashiria msukumo mpya kuelekea kuuteka mji huo mkuu wa Ukraine.

Kulingana na Maxar Technologies, sehemu ya msafara huo ambao ulionekana mara ya mwisho kaskazini-magharibi mwa Uwanja wa Ndege wa Antonov, ulio karibu.

Maxar ilisema kuwa picha zinaonyesha sehemu zingine za msafara wa kaskazini umejipanga karibu na Lubyanka, na kuweka sehemu za mizinga karibu.

Juzi, Ofisa Mkuu wa ulinzi wa Marekani, alisema vikosi vya Russia vimesogea maili tatu karibu na Kyiv katika muda wa saa 24 zilizopita.

**HABARI: BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI MADOGO NA. 262/2021**
**YUGA KIYUMBI....................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**MUSYANGI A. SAMWELI .......................MJIBU MAOMBI**

**KWA: MUSYANGI A. SAMWELI (POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa Maombi Na. 262/2021 yamepangwa kutajwa tarehe 31/03/2022 mbele ya mwenyekiti wa Baraza, R. Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 23/02/2022.

..............................................
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**BUKOBA.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO BOMANI (W) IRINGA**

**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**
**(Kanuni ya 62 kanuni za uendeshaji wa mashauri mahakama za mwanzo)**

**SHAURI LA MADAI NO 92/2021**

**MDAI.........................................GEOFREY MGIMWA**
**MDAIWA..........................YUMAHERY KIMBAVALA**

KWAMBA mdai ameleta maombi ya madai ya fedha kiasi cha Tsh3,500,000/= mbele ya mahakama hii kupitia shauri tajwa hapo juu unatakiwa kufika mbele ya mahakama hiitarehe 15/03/2022 saa 2:30 Asubuhi kwaajili ya kusikilizwa shauri hili ikiwa pamoja na kuleta mashahidi pamoja na vielelezo vinavyohusu madai hayo kwaajili ya kujitetea.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 01/03/2022

RESIDENT MAGISTRATE IRINGA
Hakimu Mkazi Mahakama ya mwanzo ya Bomani Iringa
Muhuri wa mahakama

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 27 OF 2022**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE RHOIDA KABEFU MWAKIPESILE of IPAGALA within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY EMELIA SYETE MWAKIPESILE**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15 Day of 03, 2022

**Date at Dodoma this 17TH Day of February, 2022**

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO TEMEKE**

**(TEMEKE KITUOMJUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NAMBA 24 YA MWAKA 2022**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU DINDI DONASIANS MISANYA**

**FORTUNATA FIDELIS CHIPA.............MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaj hapo juu
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 12 mwezi 04 mwaka 2022

Imesainiwa dar es salaam leo tarehe 15 mwezi 02/2022

NAIBU MSAJILI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CANTRE**

**PROBATE AND ADMNISTRATION CAUSE NO.......191 OF 2022**

**In the matter of the state of the late.............JIMSON CHARLES KIBIKI and in the matter of application for letters of administration by NURU ABDUL OMARY**

**GENERAL CITATION**
**(rule 75)**

All person claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner

Objections to the grant should be filed on or before the 31 march,2022

Dated at dar es salaam this......11 day of march,2022

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Ndg.Osmund Marcos Nichombe** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aliyoinunua kutoka kwa Ndg.Goodlove Gidion Chongolo yenye maelezo yafuatayo :
**Blue card na. : T 383 CTN**
**Aina ya gari : TOYOTA - NOAH**
**Rangi ya gari : NYEUSI**
**Chassis na. : SR 400268421**
Kwa yeyote atakayeiona anaombwa kuripoti kwenye kituo chochote cha polisi kilicho karibu.
TAARIFA YA POLISI:
**MBE/TUK/RB/430922/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**UMMY MUSTAFA MWINYIRUNGA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI (TOYOTA IST) yenye namba za usajili **T 484 DLJ**
Chassis namba: **NCP605001263**
Injini namba : **2N24270026**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi
taarifa ya polisi RB namba
**IRI/IRI/RB/81897/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HUMPHREY JOHN MNDEME** amepoteza kadi ya gari aina ya Toyota Kulger yenye namba T 119 DPF.Taarifa zimetolewa kituo cha Polisi Bukoba **KAG/BUK/RB/93843/2022.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **JOSEPHAT RAPHAEL KIBWANA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA ALLEX** yenye namba za usajili **T 871 DKH.** Yenye Engine **No: 1NZA336294** Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu.
Taarifa Polisi:
**KOR/RB/239/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Malaki Meleki Mmary**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 716 AJW** aina ya Mitsubishi Canter.
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Malaki Meleki Mmary kwa simu namba **0769582843.**
**Rbnamba/**
**SHI/SHI/RB/100181/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SAMWELI AMOSI ELIEZA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **SIMON LABAN MAKUYA** aina ya **BOXER** yenye namba za usajili **MC183 CEP.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:
**DOD/DOD/RB/100884/2022.**

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**ALOIS TITO SHAYO** anatangaza kupotelewa na hati ya Nyumba **No.57200** Plot **No.25 Block A' BAHI ROAD.** ILIYOTOLEWA NA USAJILI WA ARDHI DODOMA.Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi **DOM/RB/2579/2016.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAITON MESHACK MDYANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 717 BKX – TOYOTA RANGI YA SILVER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:
**IRI/MUF/RB/2020/2022.**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuatakama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee.

# Operesheni namba moja-**17**


**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani anampenda kwa dhati. Aliyempenda yeye kama yeye na si urembo wake.

Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

*********************************




Mshtuko ulimpata Jan. Ni kama vile alikuwa analifahamu jina hilo. Anafahamu jina la askari mwenye jina hilo. Ndiyo askari wenye majina kama hayo wako wengi, lakini huyu anayemfahamu yeye, yumo kwenye harakati hizi za kuhakikisha Diana anapatikana. Ndiyo ni Afande Marco, askari ambaye Jan anamfahamu kuwa mmoja wa wapenzi wa mpenzi wake Diana.

Alijaribu kuangaza macho. Akisaidiwa na mwaga wa taa zilizokuwa pembeni mwa barabara ya Morogoro, maeneo ya karibuni kabisa na Magomeni Mapipa. Anamfahamu fika Afande Marco. Akakumbuka jinsi alivyokwenda kumwambia atoe pesa za kumkomboa Diana kama watekaji walivyotaka na yeye akamjibu kuwa hawezi kutoa, badala yake atajua jinsi gani anaweza kukabiliana na wahalifu hao.

Pamoja na kwamba Jan alijua mmoja wa watu tishio kwenye uhusiano wake na Diana, Afande Marco ameuawa, alihuzunishwa mno na kifo hicho kwani alikuwa kwenye harakati za kumuokoa msichana huyo. Alijua sasa mpinzani wake mkubwa atabaki kuwa Challa, ambaye kwake anamuona ni hatari zaidi kuliko alivyokuwa Afande Marco. Ni kwa sababu Challa ana pesa nyingi na anaweza kufanye lolote lile. Penye udhia penyeza rupia. Pesa ilivunja mabonde na milima.

Kwa macho yake alimuona Diana akiwa kwenye gari ya watekaji ambayo ilikuwa imekuja pale kwa ajili ya makibidhiano.

Diana pia alimuona Jan, akashtuka na kuonekana kama anataka kushuka kwenye gari. Kwa ishara na macho, Jan alimtaka atulie. Alifanya hivyo, lakini macho yake hayakubanduka kwa Jan.

Alikuwa amepungua, na ile ngozi yake nyororo ya kung'aa. Kusema kweli hakuwa yule Diana aliyefahamika. Ilijulikana kwa sababu gani. Ni wiki ya tatu sasa alikuwa mikononi mwa watekaji. Hata hivyo Diana ni Diana tu. Kwa anayemuona mara ya kwanza angetetemeka kutokana na uzuri wake. Bila kujua hapo alikuwa ametoka kizuizini.

Afande mmoja alimuru Jan kupanda gari lingine, huku gari lingine likiwa na watekaji, askari pamoja na Diana. Yote mawili yalianza kuondoka kuelekea kituoni. Moja kwa moja yalitua kwenye kituo cha Polisi Magomeni. Wote walishuka na baada ya maelezo ilikuja kubainika kuwa Jan, pamoja na kwamba alionekana kuwasaidia polisi, lakini ndiye aliyewaita na ndiye aliyeweka mkoba wa pesa chini ya daraja.

"Kijana hebu tupe taarifa kidogo ili tujue jinsi gani ya kuiripoti kwa wakubwa zetu, ilikuwaje mpaka ukatupigia simu kuwa kuna tukio, halafu wewe ndiye uliyeweka mkoba wa pesa pale, pia kufanya kazi ya kutusaidia kuwaua baadhi ya watekaji?" Aliuliza afande mmoja aliyeonekana kuwa mkuu wa kituo.

Jan alikuwa na mkuu huyo ofisini peke yao. "Aliyetekwa ni mpenzi wangu." Kwa mara ya kwanza Jan aliongea ukweli kuhusu Diana. Hakusema tena kama ni mpwa wake kama alivyokuwa akijitambulisha huko nyuma, hasa wakati wa uhai wa Afande Marco.

"Kwa hiyo afande, mara kwa mara watekaji huwa wanatupigia simu kutaka pesa na walikuwa wanahitaji shilingi milioni hamsini. Mara ya kwanza tuliweka chini ya daraja la Mfugale, lakini hawakuja kuchukua kwa kushtuka kuwa tumewaambia askari. Wao walituonya kuwa tusiwaambie askari. Wakatishia kutaka kumuua Diana, lakini wakatupa nafasi ya mwisho kuwa sasa tukaweke hizo pesa chini ya daraja la Kajima, Magomeni Mapipa." Jan alifunguka.

"Nani aliyekuwa akienda kuweka mkoba wa pesa kote huko?"

"Ni mimi afande."

"Tulipofungua mkoba ule ambao watekaji walikuja kuuchukua, hatukukuta pesa yoyote zaidi ya karatasi nyingi zilizokatwakatwa kama pesa, ni kwa nini?" Afande akauliza tena.

"Ni kwa sababu hatukuwa na pesa hizo ambazo walizitaka. Ni kweli tulikuwa tunafanya mchezo wa hatari, lakini ilibidi tuwaongopee tu kwa sababu hatukuwa na la kufanya na ilikuwa ni lazima tumuokoe Diana kwa ujanja wowote ule."

"Upo wewe na nani ambao mlikuwa mnaandaa yote haya?"

"Ni mimi na mjomba wake Diana. Yote haya tulikuwa tuyandaa nyumbani kwake Ubungo."

Jan kwa asilimia kubwa alikuwa anaongea ukweli, lakini mengine alipindisha kidogo.

Ukweli ni kwamba mpango mzima wa kuweka makaratasi kwenye mkoba ambao uliwekwa chini ya daraja mara mbili, ulikuwa ni wa kwake na hakumjulisha mjomba Ken.

**Walichokubaliana na Ken ni kuweka kwenye mkoba shilingi milioni 15 ambazo zilipatikana kutoka kwa Challa. Ambacho Ken hakijui, ni kwamba Jan alizichukua pesa hizo na kwenda kuziweka nyumbani kwake, na kujaza makatarasi matupu.**

Walichokubaliana na Ken ni kuweka kwenye mkoba shilingi milioni 15 ambazo zilipatikana kutoka kwa Challa. Ambacho Ken hakijui, ni kwamba Jan alizichukua pesa hizo na kwenda kuziweka nyumbani kwake, na kujaza makatarasi matupu.

Kikubwa ni kwamba Jan hakutaka watekaji wale wachukue mkoba na kumuacha Diana bila kukamatwa. Na ndiyo maana awali alikwenda kumtaarifu Afande Marco, na mara ya pili aliwapigia maafande wa kituo cha Polisi Magomeni waje kwenye tukio. Alijua kama wangeuchukua mkoba na kwenda kukuta hakuna pesa, basi hiyo peke yake ingekuwa tiketi ya kifo cha Diana. Kama wakikamatwa hata kama mkoba utakuwa na makaratasi haitakuwa na hatari yoyote. Na kama alivyotarajia ndivyo ilivyokuwa.

"Kwa nini ulipoweka mkoba haukuondoka na badala yake ukaamua na wewe kujiweka kwenye hatari, wakati tayari ulikuwa umeshatuambia twende kwenye eneo la hatari? Huoni kama ulikuwa unahatarisha maisha yako?" Afande alizidi kummiminia maswali Jan.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# NYOTA BERKANE AIPA YANGA UBINGWA BARA

**Na Shufaa Lyimo**

WINGA wa RS Berkane, Fiston Abdulrazak, amesema mpaka sasa hajaona mpinzani wa Yanga katika vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania msimu huu wa 2021/2022.

Fiston pia aliliambia gazeti hili anafurahishwa na kiwango kinachoonyeshwa na Mkongomani mwenzake, Fiston Mayele pamoja na Mrundi, Said Ntibazonkiza.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Fiston alisema kiwango kinachoonyeshwa na Yanga msimu huu ni kikubwa tofauti na kilivyokuwa msimu uliopita.

Fiston alisema Yanga imekuwa ikipambana katika kila mechi kwa kuwa inahitaji kutimiza malengo yake ya kutwaa ubingwa msimu huu baada ya kuukosa kwa misimu minne mfululizo.

"Kwa kweli mpaka sasa hivi sijaona mpinzani wa kuishusha Yanga hapo kilelemi, sijaona timu ya kuizuia ili isipate ubingwa, inajitahidi na inapambana kufanya vizuri katika kila mchezo inayocheza," alisema Fiston, nyota huyo wa zamani wa vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mchezaji huyo alisema anaifuatilia mara kwa mara timu hiyo yenye makao yake makuu Mtaa wa Twiga na Jangwani na kugundua imefanya usajili mzuri ambao unawapa mafanikio katika msimu huu.

"Kitu ambacho ninaona kinazidi kuleta ushindani kwenye timu ya Yanga ni hali ya utulivu, viongozi walitulia kuanzia katika kufanya usajili kwa kuongeza wachezaji wenye viwango vya juu," Fiston alisema.

Aliongeza ushindani wa kuwania namba na usajili wa wachezaji wazoefu akiwano Mayele na Ntibazonkiza umesaidia kuipa Yanga matokeo chanya katika michezo yake yote ya mzunguko wa kwanza.

"Namkubali sana Nitabazonkiza na Mayele kutokana na ubora waliokuwa nao, ni wachezaji wanaozungumzwa na kufuatiliwa na wadau wengi wa soka Afrika," aliongeza winga huyo.

Yanga inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 42 wakati mabingwa watetezi, Simba walioko katika nafasi ya pili wana pointi 34, timu zote zikiwa zimecheza mechi 16.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk.Damas Ndumbaro (katikati) akiwa na Mkurugenzi wa Biashara ya Kimataifa ya Atletico Madrid, Danilo Scio (wa pili kulia). Wengine ni Balozi wa Tanzania nchini Uhispania mwenye makazi yake jijini Paris, Ufaransa (wa pili kushoto) na Samuel Shelukindo (wa kwanza kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Atletico, Getafe kuinadi Tanzania

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro amefanya mazungumzo na uongozi wa Atletico Madrid na Getafe zinazoshiriki Ligi Kuu Hispania (Laliga) kwa lengo la kuitangaza Tanzania hususani katika sekta ya utalii.

Pia, amefanya mazungumzo na klabu ya Real Valladolid ya nchini huko ambayo inamilikiwa na mchezaji wa zamani wa Brazil, Ronaldo De Lima.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii jana imesema Dk.Ndumbaro alikutana kwa nyakati tofauti na viongozi wa vilabu hivyo vya mpira vyenye mashabiki wengi Hispania na duniani.

Waziri huyo alisema katika mazungumzo hayo viongozi wote wa timu hizo wameonyesha utayari wa kushirikiana katika kuitangaza Tanzania kiutalii.

"Mazungumzo haya ni moja ya jitihada za kuhakikisha vivutio vya utalii vya Tanzania vinajulikana duniani kupitia michezo kwa kutangazwa kupitia matangazo ya kwenye jezi ya vilabu pamoja na mbao za matangazo zilizopo uwanjani."

Aliongeza: "Shabaha yetu kubwa kama nchi ni kuhakikisha tunafungamanisha utalii na michezo kwa kutumia timu kubwa za mpira kwa lengo la kuwavutia watalii wengi zaidi kuja nchini Tanzania".

AlisemaTanzania inategemea utalii wa wanyamapori kwa asilimia 100 hivyo kupitia mkakati wa kutumia michezo vivutio vingine vya utalii kama vile utalii wa fukwe, utalii wa utamaduni pamoja na utalii wa ikolojia utaweza kujulikana na dunia kote na hivyo watalii kuanza kumiminika kuja nchini.

## Mafunzo, Mlandege KMKM, JKU mzigoni

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KIKOSI cha Maafande wa Mafunzo kimesema kinatarajia mchezo wao wa Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya Mlandege utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan utakuwa mgumu na wenye ushindani, lakini wamejipanga kupata ushindi.

Kocha Msaidizi wa Mafunzo, Abdallah Bakari 'Kocha Edo' alisema wamejipanga kuendelea kupambana katika michezo yote iliyosalia na hatua ya lala salama kwa sababu wanahitaji kufikia malengo yao.

Edo alisema amekiandaa vyema kikosi chake na anaamini watapata matokeo chanya ili wajiimarishe katika msimamo wa ligi hiyo.

"Ninawakumbusha wachezaji wangu kucheza kwa hamasa kubwa kama ilivyokuwa hapo awali na kusahau matokeo mabaya ya michezo iliyopita," Edo alisema.

Aliongeza kupoteza michezo miwili mfululizo ilichangia kuwavunja moyo kuelekea mbio za ubingwa lakini anawaomba mashabiki kushikamana ili wapate ushindi.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan kuanzia saa 1:00 usiku itakuwa ni kati ya Mabaaria wa KMKM dhidi ya JKU.

## Maulid aongoza magoli Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI mabao 346 yamefungwa kati ya michezo 163 iliyochezwa ya Ligi Kuu Zanzibar, mshambuliaji wa Maafande wa KVZ, Maabad Maulid, anaongoza katika orodha ya wafungaji kwa kupachika magoli 14

Maulid amefunga mabao hayo katika michezo 21 aliyocheza huku katika orodha hiyo anafuatiwa na Abdulkarim Yunus Idd wa JKU mwenye mabao 10 wakati nafasi ya tatu inashikiliwa na Optatus Yustine wa KMKM mwenye magoli tisa.

Wengine waliokuwapo katika tano bora kwa kupachika magoli ni Abdulnasir Asaa wa Mlandege ambaye ana magoli nane, Abrahaman Othman (KMKM), Ali Khatib Juma (Mafunzo), Mundhir Abdalla (Kipanga) na Rashid Ali wa Polisi ambao kila mmoja ana magoli saba.

Akizungumza na gazeti hili ,Maulid alisema malengo yake makubwa ni kuhakikisha anaibuka mfungaji bora katika msimu huu na kujiwekea rekodi nzuri.

"Nataka nitimize ndoto yangu ya kuwa mfungaji bora wa msimu huu tena, ili nitimize ndoto yangu lazima niongeze juhudi na tuendelee kufanya vizuri katika timu yangu," alisema Maulid.

Aliongeza yeye na wachezaji wenzake wanaahidi kupambana ili kuipatia timu yao taji la Ligi Kuu Zanzibar msimu huu kwa sababu ya kulikosa kwa muda mrefu.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE APELEKWA ENGLAND
MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, anapaswa kujiunga na Liverpool au Manchester City, amesema mlinzi wa zamani wa Ligi Kuu England, Micah Richards. ***(Liverpool Echo)***

### NEYMAR APINGA MZOZO
MSHAMBULIAJI nyota wa Brazil, Neymar amepinga ripoti ya kuzozana na mchezaji wa kimataifa wa Italia na mchezaji mwenzake wa Paris St-Germain, Gianluigi Donnarumma mwenye umri wa miaka 23, baada ya timu yao kuondolewa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Real Madrid. ***(Mirror)***

### DYBALLA ATAKA KUONDOKA
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 28 anaamini Juventus itamruhusu kuondoka ifikapo msimu wa joto. ***(Gazetta dello Sport)***

### POCHETTINO ATOA MASHARTI
KOCHA wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino anataka Manchester United kumhakikishia atakuwa chaguo lao la kwanza akiamua kuchukua usukani Old Trafford. ***(Mail)***

### FLETCHER AGEUKA MPATANISHI
MKURUGENZI wa Ufundi wa Manchester United, Darren Fletcher anasemakana kuhudumu kama mpatanishi wa nyuma ya pazia wa klabu hiyo kutokana taharuki inayoshuhudiwa katika chumba cha kubadilisha nguo. ***(Sun)***

### TUCHEL ANUKIA UNITED
MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich anayekabiliwa na vikwazo vya serikali ya Uingereza ameipatia Manchester United nafasi ya kumsajili kocha, Thomas Tuchel, kwa mujibu wa beki wa zamani wa Liverpool, Jamie Carragher. ***(Telegraph)***

### TISA KUONDOKA CHELSEA
CHELSEA ina wachezaji tisa ambao mikataba yao inamalizika msimu huu wa joto na huenda wakaondoka bila malipo baada ya serikali ya Uingereza kumwekea vikwazo mmiliki wake, Roman Abramovich. ***(Metro)***

### RUDIGER SAFARI IMEIVA
MKATABA wa beki wa Ujerumani, Antonio Rudiger katika klabu ya Chelsea unamalizika msimu huu wa joto na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 anajiandaa kuondoka baada ya The Blues hao kukosa nafasi kadhaa za kumpatia mkataba mpya ***(Sky Sports News, via Star)***


### PULISIC ANUKIA JUVENTUS
JUVENTUS wanatafakari uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa Chelsea na Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 23 msimu huu wa joto. ***(Gazetta dello Sport)***

### DALOT, UNITED KUTETA
KLABU ya Manchester United wanapanga kuanza mazungumzo na mlinzi wa Ureno, Diogo Dalot kuhusu mkataba mpya, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 akisalia na miezi 18 katika mkataba wake wa sasa. ***(Teamtalk)***

### JUVENTUS, MILAN VITANI
KLABU za Italia AC Milan na Juventus zinatathmini uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa Lille na Timu ya Taifa ya Ureno, Renato Sanches mwenye miaka 24. ***(Goal)***

### GIL KUTUA VALENCIA
VALENCIA wanataka kumsajili winga wa Tottenham Hotspur, Bryan Gil mwenye umri wa miaka 21 kwa mkopo msimu ujao na huenda wakamwongeza mwaka mmoja raia huyo wa Hispania. ***(Star).***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA, UNITED MAMBO MAGUMU

Mazungumzo na kiungo huyo Mfaransa bado yamezungukwa na sintofahamu zikiwa...

**MANCHESTER, England**

WAKATI Manchester United wakiwa wamebakiza michezo 10 tu kuhitimisha msimu wa 2021/22 kwenye Ligi Kuu England, hakuna jipya kuhusu mkataba mpya kwa kiungo wao, Paul Pogba.

Pogba anaelekea kumaliza mkataba wake wa miaka mitano hapo Manchester United mwishoni mwa msimu huu na kwa hali ilivyo, hakuna maongezi ya mkataba mpya tangu Julai, mwaka jana.

Inaripotiwa uongozi wa United ulimpatia ofa ya mkataba mpya, Pogba na wakala wake, hawakujibu chochote kuhusu ofa hiyo.

Hii ni hali inayozua sintofahamu kuhusu mchezaji huyo ambaye pia, anahusishwa na PSG na Real Madrid.

Ingawa haijafahamika wazi kama lengo la Pogba ni kuondoka kama mchezaji huru au anachagiza maboresho zaidi kwenye mkataba aliopewa au lengo lake hasa ni lipi.

Yote kwa yote, United ina kazi kubwa ya kufanya katika maboresho ya kikosi chake mwishoni mwa msimu huu.

Kumpata kocha mpya wa muda mrefu, kuuza baadhi ya wachezaji, kununua wachezaji wapya, kuboresha mifumo ya uongozi wa klabu chini ya uongozi wa mkurugenzi mpya ndio vipaumbele kulekea majira ya joto.

LIVE IN PLAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,013

MECHI KALI

MANCHESTER UTD

VERSUS

TOTTENHAM

1 | 2.22

X | 3.41

2 | 3.17

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa

1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi

00. Toka

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:

18+ 0764115588, 0677115588

0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# NEYMAR, DONNARUMMA NUSURA WAZICHAPE

**MADRID, Hispania**

NEYMAR na golikipa, Gianluigi Donnarumma ilibidi watenganishwe na wachezaji wenzao wa Paris Saint-Germain katika vyumba vya kubadili nguo, baada ya wawili hao kutaka kupigana.

Sababu ya wachezaji hao kutaka kupigana ni kutokana na hasira kwa kufungwa 3-1 na Real Madrid na kuondolewa katika Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Neymar na Donnarumma walikuwa wamepata pigo kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Hispania na ilionekana kila mmoja akimshutumu mwenzake.

Mara baada ya mchezo huo, wachezaji hao walionekana kuzozana kwa maneno makali.

Kwa mujibu wa ripoti, Neymar alikuwa akimlaumu Donnarumma kwa makosa yake yaliyoigharimu timu na Real Madrid kupata bao la kusawazisha kipindi cha pili.

Na golikipa huyo wa kimataifa wa Italia alijibu mapigo kwa kumlaumu Neymar kupoteza mpira wa Karim Benzema kwa bao la pili.

Lakini hakukuwa na tukio hilo pekee kwenye mchezo huo, kwani hata Rais wa PSG, Nasser Al-Khelaifi na Mkurugenzi wa Michezo, Leonardo walikwenda kwenye chumba cha waamuzi na kumshutumu mwamuzi kwa kutotoa faulo baada Benzema kumchezea faulo Donnarumma.

Al-Khelaifi ameripotiwa kumtisha mwamuzi kwa kumfokea "Nitakuuwa" kabla ya polisi na walinzi wengine kutokea na kumaliza tukio hilo.

# Chelsea yaathiriwa na vikwazo

**LONDON, England**

MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich na mali zake zote ambazo ziko ndani ya Uingereza zimeshikiliwa na serikali ya nchi hiyo kutokana na kuwa karibu na Rais wa Russia.

Serikali ya Uingereza inadai Roman Abramovich anahusika na siasa za Vladimir Putin, aliiweka sokoni klabu yake ili kuinusuru, lakini kutokana na vikwazo alivyowekewa hataweza kuiuza klabu hiyo bila ya kupata uthibitisho kutoka serikalini.

Vikwazo hivyo ni sehemu ya majibu yake kwa uvamizi wa Russia dhidi ya Ukraine.



Yeye ni mmoja wa wafanyabiashara saba matajiri kuwekewa vikwazo vipya, ikiwa ni pamoja na kuzuiliwa kwa mali yao na marufuku ya kusafiri.

Orodha hiyo pia inajumuisha mabilionea Igor Sechin na Oleg Deripaska, wote wanaoonekana kuwa washirika wa Putin.

Waziri Mkuu wa England, Boris Johnson alisema "hakuwezi kuwa na maeneo salama" kwa wale ambao wameunga mkono uvamizi huo.

Klabu ya chelsea haitaweza kuuza mchezaji au kununua mchezaji yeyote wala kuwapatia mikataba mipya kwa wachezaji waliomaliza muda wao kwenye klabu hiyo.

Pia hawataweza kuuza tiketi zingine isipokuwa zile zilizouzwa kwa msimu mzima.

Pia Chelsea haitaruhusiwa kupata mapato ya hatimiliki ya matangazo ya television ina maana klabu hiyo inaweza kupitia kipindi kigumu kwenye kulipa mishahara ya wachezaji na itabidi waanze kuwapigia mahesabu wachezaji makinda ambao wapo kwenye vilabu vingine kwa mkopo kama Armando Broja na Conor Gallagher.

## HABARI MICHEZO


# 3,643,920

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/03/22 | 18:00 | Millwall vs Middlesbrough | 2.22 | 3.20 | 3.15 |
| 02. 12/03/22 | 18:00 | Coventry vs Sheffield Utd | 2.60 | 3.14 | 2.65 |
| 03. 12/03/22 | 18:00 | Blackpool vs Swansea | 2.36 | 3.29 | 2.85 |
| 04. 12/03/22 | 19:00 | Montpellier vs Nice | 3.02 | 3.47 | 2.24 |
| 05. 12/03/22 | 23:00 | Troyes vs Nantes | 2.63 | 3.22 | 2.68 |
| 06. 12/03/22 | 23:00 | Getafe vs Valencia | 2.46 | 3.06 | 3.06 |
| 07. 12/03/22 | 23:30 | Belenenses vs Boavista | 2.71 | 3.25 | 2.51 |
| 08. 13/03/22 | 14:15 | Fortuna Sittard vs Willem II Tilburg | 2.80 | 3.35 | 2.48 |
| 09. 13/03/22 | 15:00 | Luton Town vs QPR | 2.25 | 3.20 | 3.10 |
| 10. 13/03/22 | 15:30 | Hannover vs Nurnberg | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 11. 13/03/22 | 17:00 | Angers vs Reims | 2.27 | 3.13 | 3.28 |
| 12. 13/03/22 | 17:00 | Strasbourg vs Monaco | 2.37 | 3.32 | 2.92 |
| 13. 13/03/22 | 17:00 | Everton vs Wolverhampton | 2.29 | 3.26 | 3.16 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" – NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" – NI TIMU KUTOKA SARE
"2" – NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 12/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2004 | Ufa vs Nizhny Novgorod | 2.10 | 3.04 | 3.63 |
| 15:30 | 4135 | Brighton vs Liverpool | 5.81 | 4.51 | 1.50 |
| 15:30 | 4583 | Barnsley vs Fulham | 6.28 | 4.32 | 1.45 |
| 16:00 | 4118 | Kasimpasa vs Caykur Rizespor | 1.62 | 3.94 | 4.93 |
| 16:00 | 4657 | Mbeya City vs Kagera Sugar | 2.06 | 2.88 | 3.75 |
| 16:00 | 5055 | Levante vs Espanyol | 2.28 | 3.40 | 3.05 |
| 16:30 | 3366 | Arsenal Tula vs Dinamo Moscow | 4.62 | 3.64 | 1.70 |
| 17:00 | 1323 | Spezia vs Cagliari | 2.66 | 3.26 | 2.66 |
| 17:00 | 3311 | Salernitana vs Sassuolo | 3.96 | 4.01 | 1.79 |
| 17:30 | 1994 | Union Berlin vs Stuttgart | 2.08 | 3.43 | 3.43 |
| 17:30 | 3897 | SC Freiburg vs VfL Wolfsburg | 2.11 | 3.43 | 3.33 |
| 17:30 | 4239 | Hoffenheim vs Bayern Munchen | 4.38 | 4.88 | 1.58 |
| 18:00 | 1318 | Coventry vs Sheffield Utd | 2.70 | 3.14 | 2.55 |
| 18:00 | 1570 | Millwall vs Middlesbrough | 2.85 | 3.10 | 2.46 |
| 18:00 | 1815 | Peterborough vs Stoke City | 3.48 | 3.28 | 2.05 |
| 18:00 | 1921 | Nottingham vs Reading | 1.57 | 3.94 | 5.32 |
| 18:00 | 2212 | Blackburn vs Bristol City | 1.71 | 3.54 | 4.71 |
| 18:00 | 3634 | Brentford vs Burnley | 2.15 | 3.25 | 3.50 |
| 18:00 | 3722 | Blackpool vs Swansea | 2.29 | 3.23 | 2.99 |
| 18:00 | 3765 | Bournemouth vs Derby | 1.55 | 3.83 | 5.70 |
| 18:00 | 4373 | Birmingham vs Hull City | 2.12 | 3.24 | 3.34 |
| 18:00 | 4820 | Cardiff vs Preston | 2.33 | 3.10 | 3.05 |
| 18:15 | 1669 | Granada vs Elche | 2.25 | 3.25 | 3.25 |
| 18:15 | 2860 | Mechelen vs Charleroi | 2.36 | 3.36 | 2.82 |
| 18:30 | 1081 | Sparta Rotterdam vs GO Ahead Eagles | 1.91 | 3.35 | 3.89 |
| 19:00 | 1337 | Trabzonspor vs Goeztepe | 1.60 | 3.91 | 5.14 |
| 19:00 | 3925 | Lokomotiv Moscow vs CSKA Moscow | 3.14 | 3.14 | 2.26 |
| 19:00 | 3964 | Coastal Union vs Ruvu Shooting | 2.11 | 3.00 | 3.95 |
| 19:00 | 5243 | Montpellier vs Nice | 3.04 | 3.34 | 2.29 |
| 20:00 | 3961 | Sampdoria vs Juventus | 4.94 | 3.70 | 1.70 |
| 20:00 | 4181 | FC Zurich vs St. Gallen | 1.76 | 4.05 | 3.85 |
| 20:30 | 1190 | Zulte Waregem vs Eupen | 2.37 | 3.41 | 2.77 |
| 20:30 | 1730 | Monchengladbach vs Hertha BSC | 1.57 | 4.48 | 4.87 |
| 20:30 | 2606 | Cercle Brugge vs Kortrijk | 1.66 | 3.76 | 4.84 |
| 20:30 | 4869 | Villarreal vs Celta Vigo | 1.66 | 3.95 | 4.90 |
| 20:30 | 5249 | Manchester Utd vs Tottenham | 2.22 | 3.41 | 3.17 |
| 20:45 | 1729 | Groningen vs NEC Nijmegen | 1.85 | 3.44 | 4.03 |
| 21:00 | 1129 | FC Arouca vs Pacos Ferreira | 2.45 | 3.05 | 2.95 |
| 21:00 | 1616 | New York City vs Montreal Impact | 1.41 | 4.51 | 7.62 |
| 21:30 | 1886 | Columbus Crew vs Toronto FC | 1.60 | 4.10 | 5.21 |
| 21:30 | 5892 | Inter Miami CF vs Los Angeles FC | 3.85 | 3.75 | 1.87 |
| 22:30 | 4395 | FC Sion vs FC Lugano | 2.84 | 3.09 | 2.50 |
| 22:45 | 4450 | Oostende vs Brugge | 6.50 | 4.73 | 1.41 |
| 22:45 | 4723 | Hearts vs St Mirren | 1.71 | 3.49 | 4.36 |
| 22:45 | 5823 | AC Milan vs Empoli | 1.37 | 5.01 | 7.61 |
| 23:00 | 1058 | Waalwick vs Heerenveen | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 23:00 | 3199 | Troyes vs Nantes | 2.94 | 3.13 | 2.47 |
| 23:00 | 5685 | Getafe vs Valencia | 2.35 | 3.10 | 3.20 |
| 23:30 | 2563 | Seattle Sounders vs LA Galaxy | 2.06 | 3.31 | 3.66 |
| 23:30 | 5439 | Belenenses vs Boavista | 3.26 | 3.11 | 2.24 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# SERIKALI YAIBATIZA RASMI U-17 JINA SERENGETI GIRLS

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17, ambayo inajiandaa na mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia dhidi ya yosso wenzao wa Botswana, imepewa rasmi jina la Serengeti Girls.

Hiyo ni baada ya kikosi cha umri huo cha wavulana kujulikana kwa jina la Serengeti Boys.

Waziri ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, alitoa jina hilo jana alipotembelea mazoezi ya timu hiyo iliyoko chini ya Kocha Mkuu, Bakari Shime yanayofanyika kwenye Uwanja wa Amaan kila siku.

Mchengerwa alisema timu hiyo itaendelea na kambi yake visiwani hapa kutokana na mwamko mkubwa uliokuwepo katika mechi yao ya kwanza ambapo Serengeti Girls ilipata ushindi mnono wa mabao 7-0.

Alisema Wazanzibar na Watanzania wameonyesha mapenzi na utayari wa hamasa kwa timu yao hali inayopelekea timu hiyo kufanya vizuri huku akisisitiza wachezaji hao kuwa na nidhamu ndani na nje ya uwanja.

"Tunataka mpambane kwa kila kibarua mtakayofika, mcheze kwa uchungu ili mfanye vizuri, Watanzania tupo nyuma yenu, hatutowaangusha kwa kila hatua nzuri mtakayopiga, nina imani tutafanya vizuri," alisema Mchengerwa.

Akiwasilisha salamu za Rais, Samia Suluhu Hassan, waziri huyo alisema Watanzania wanamatumaini makubwa kwa timu hiyo kufuzu kucheza kombe la dunia.

Pia ameishukuru Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF) kwa ushirikiano unaoendelea na kufanikisha kambi hiyo inakamilisha programu zake.



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa (katikati), akiwa na viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Shirikisho la mchezo huo Zanzibar (ZFF) na wachezaji wa Serengeti Girls baada ya mazoezi ya timu hiyo kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar jana. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# Kuogelea wapata ugeni mkubwa

**Na Saada Akida**

RAIS wa Shirikisho la Kuogelea la Kimataifa (FINA), Husain Al Musallam, anatarajiwa kuwasili nchini keshokutwa ambapo ataambatana na kiongozi wa juu wa Afrika, Sam Ramasamy.

Ramasamy pia ni Makamu rais wa FINA mbali yakuwa rais wa Afrika wa shirikisho la mchezo huo (CANA).

Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Kuogelea Tanzania (TSA), Asmah Hilal, alisema msafara wa viongozi hao utakuwa na watu tisa, akiwamo Chaykh Ahmad Al Saab ambaye Msaidizi wa Rais wa FINA, Alex Szanto (FINA jumbe) na Mikolaus Schonfeldt ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji Msaidizi wa FINA.

Asmah aliwataja maofisa wengine wanaokuja ni bingwa wa zamani wa Olimpiki, Ferry Weertam na Ranom Kromowidjojo ambaye ni bingwa wa zamani wa dunia na Olimpiki.

Alisema ujio wa uongozi wa juu wa mchezo huo ni heshima kubwa kwa Tanzania kwa sababu hii ni mara ya kwanza kihistoria.

"Mara baada ya kuwasili (Jumatatu mchana), watakwenda moja kwa moja kuangalia mazoezi ya waogeleaji katika bwawa la kuogelea la Champion Rise na baadaye watashiriki kikao cha pamoja na wadau, viongozi wa serikali, Kamati ya Olimpiki na wenyeji TSA kitakachofanyika kwenye ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere," alisema Asmah.

Aliongeza ugeni huo utaondoka jijini Dar es Salaam Jumanne na kuelekea Zanzibar ambapo watakutana na Rais, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Michezo
Jumamosi Machi 12, 2022
Nipashe



## Pogba, United mambo magumu

# PABLO AFUNGUKA SIMBA SC IMETIMIA

### ●●●Huku nyota wake wakiahidi kuleta furaha kwa kuzibakisha pointi…

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco akifurahishwa na kurejea kwa wachezaji wake waliokuwa majeruhi wa muda mrefu, nyota wa Simba wameahidi kupambana na kuvuna pointi tatu katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya RS Berkane itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Nyota waliokuwa majeruhi na sasa wamejerea kikosini tayari kwa mapambano ni pamoja na beki, Thadeo Lwanga na mshambuliaji Mzalendo, Kibu Denis, Chris Mugalu, Sadio Kanoute, Jonas Mkude na Aishi Manula.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohamed Hussein (Zimbwe Jr), aliliambia gazeti hili jana wamejiandaa vizuri na wako tayari kupambana kupata ushindi katika mchezo huo ambao wanatarajia utakuwa na ushindani.

Beki huyo alisema kurejea kwa wachezaji waliokuwa majeruhi wameongeza nguvu kubwa katika kikosi chao na kilichobakia ni kujituma ili kuhakikisha wanawapa furaha wanachama na mashabiki wao hapo kesho.

"Unapojiandaa na mechi ngumu ya kimataifa inakuwa vizuri kuwa na kikosi kamili, kocha anakuwa na wigo mpana wa kupanga timu. Tunaenda katika mchezo mgumu jambo la kushukuru tunaenda tukiwa na kikosi kamili," alisema Zimbwe Jr.

Aliongeza wanahitaji kupata pointi tatu ni muhimu kwao kwa sababu zitawaweka katika mustakabali mzuri wa kundi hilo na kuongeza morali kuelekea mechi mbili zilizosalia za hatua hiyo.

Naye beki mkongwe, Erasto Nyoni amewaomba mashabiki wa Simba kujitokeza kwa wingi uwanjani kuipa sapoti timu yao katika mchezo huo ili kuwaongezea nguvu ya kupambana.

"Tunahitaji pointi tatu muhimu nyumbani, maandalizi yetu ni mazuri na benchi la ufundi linaona mapungufu tunayofanya kila mechi na kuyafanyia kazi, kikubwa nawaomba mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi uwanjani kutupa sapoti tunaamini tutawapa furaha," alisema Nyoni.

Alisema wanatambua mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa lakini wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaendelea kulinda rekodi nzuri ya kupata matokeo chanya katika michezo yao ya kimataifa wanapokuwa kwenye uwanja wa nyumbani.

Pablo alisema walicheza katika mazingira magumu ugenini mechi zao mbili zilizopita dhidi ya US Gendamarie na RS Berkane na wanashukuru kwa kupata pointi moja, kutokana na idadi kubwa ya majeruhi aliyokuwa nayo.

"Nimefurahi sana, kurejea kwao kumetanua wigo wa kuwa na wachezaji wengi wa kuchagua kucheza na hata wakati wa kubadilisha wachezaji una uhakika na anayeingia, Kibu na Lwanga wataongeza kitu Jumapili. Hata kama hawatoanza kwa sababu hawajakuwa na utimamu wa mwili kwa asilimia zote mia moja, lakini nguvu yao inaweza kuhitajiwa kipindi cha pili," alisema Pablo.

Kuelekea mechi ya kesho, Pablo alisema wameyafanyia kazi mapungufu hasa ya kufungwa mabao ya faulo ambayo ndiyo yaliyowapa ushindi RS Berkane katika mechi iliyopita.

"Tunawaomba mashabiki kujitokeza katika mechi ya Jumapili, lakini si hii ya kimataifa, waje pia kutushangilia kwenye mechi za Ligi Kuu, katika mechi iliyopita dhidi ya RS Berkane tulikuwa na matatizo mengi, pasi zilikuwa zinapotea, nadhani kutokana na uwanja haukuwa mzuri, tulikuwa dhaifu kwenye mipira iliyokufa na tuliwapa kona nyingi, lakini pia hatukushambulia vizuri, inawezekana kwa sababu tulikuwa ugenini. Sasa tuko nyumbani na itakuwa mechi muhimu kwetu kushinda ili kujiweka vyema kwenye hatua inayofuata," Pablo alisema.

Wachezaji ambao hawako katika mipango ya mechi ya kesho ni Clatous Chama ambaye anabanwa na kanuni pamoja na Hassan Dilunga na nahodha, John Bocco kwa sababu ni majeruhi.



Winga wa Simba, Bernard Morrison (kulia) akiwania mpira dhidi ya kiungo wa timu hiyo, Rally Bwalya wakati wa mazoezi ya kuelekea mechi ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya RS Berkane kutoka Morocco itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

## Nabi auchambua ubingwa Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Yanga kikishuka dimbani leo kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Timu ya Soka ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 23 ya Somalia, Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi amesema hatadharau mechi yoyote iliyoko mbele yake.

Mechi hiyo ya kirafiki inachezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam ikiwa na lengo la kuchangia mfuko wa Taasisi ya Ally Kimara.

Pia ni sehemu ya maandalizi kuelekea mchezo wao ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC utakaochezwa Machi 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema wamejipanga kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mechi zote kwa sababu wanaamini pointi ndio zitawafanya wafikie malengo.

Nabi alisema amewaandaa wachezaji wake kupambana na kuiona kila mechi sawa na fainali, hivyo wanahitaji ushindi na si matokeo mengine tofauti.

"Ili uwe bingwa ni lazima ushinde, uwe na pointi nyingi, sisi malengo yetu ni kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu na mashindano ya Kombe la FA, tunajua kuna ushindani, tuko tayari kwa kila changamoto iliyoko mbele yetu," alisema Nabi.

Aliongeza bado hakuna timu yenye uhakika na nafasi iliyopo, kutokana na idadi ya mechi zilizosalia.

"Mechi zilizobaki ni nyingi, ni mapema sana kusema nani amekaribia ubingwa na nani atashuka daraja, tunachokifanya sasa ni kuendelea kujiimarisha ili tupate ushindi na si kuangalia kitu kingine," Nabi aliongeza.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Haji Manara alisema klabu hiyo imekubali kucheza mechi hiyo kwa ajili ya kurejesha hisani kwa jamii lakini pia kuwafanya wachezaji wao waendelee kuwa na 'moto' wakati huu ambapo hawana mechi ya ligi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >